Ijumaa Machi 8, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 - Na. 0579860

www.ippmedia.com

.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Askari JWTZ matatani kwa tuhuma za ujambazi

UKURASA 3

UKURASA 13

# Nderemo, vifijo Mbowe kuachiwa kwa dhamana

• **Jaji** aonya mahakama za chini kuacha kuchezea haki, ashangazwa na washtakiwa kufutiwa dhamana, asema... *Ukurasa 2*





Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, wakipongezwa na wanachama na viongozi mbalimbali wa chama hicho, baada ya kushinda rufani ya dhamana katika Mahakama Kuu, jijini Dar es Salaam jana. **Picha ya juu;** Mbowe na Matiko, wakipongezana baada ya uamuzi kutolewa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### HATIMAYE UGONJWA KIMETA WADHIBITIWA

SERIKALI imesema mlipuko mpya wa ugonjwa wa kimeta katika wilaya za Moshi, Rombo mkoani Kilimanjaro na Longido mkoani Arusha...

## Kortini tuhuma biashara binadamu

UKURASA 3

## Aliyosema Kibonde kuashiria kifo chake



UKURASA 2

MICHEZO **ZAHERA: YANGA HAITAYUMBA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Nderemo, vifijo dhamana ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

SHANGWE, vifijo na nderemo vilitawala jana katika ukumbi namba moja wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, kuachiwa kwa dhamana.

Wafuasi wa Chadema walishikwa na furaha baada ya Jaji Sam Rumanyika kutamka kuwa "walalamikaji kuanzia sasa waachiwe huru kwa dhamana, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu si tu ilikosea bali wakati wake ulikuwa bado kama ni mtoto basi ni njiti".

Hatua hiyo ilisababisha wafuasi hao kushindwa kuvumilia kusubiri Jaji Rumanyika kutoka ndani ya ukumbi kwa kuwa baada ya tamko hilo, walilipuka kwa vifijo huku wengine wakishangilia.

Baada ya Jaji kutoa uamuzi huo wa rufani ya kupinga Mbowe na Matiko kufutiwa dhamana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baadhi ya viongozi na wafuasi wa Chadema waliwakumbatia warufani hao wakiwa kizimbani.

Katika kuonyesha kuwa kesi hiyo ilikuwa ikivuta hisia za watu wengi, ilipofika saa 6:30 mchana, ukumbi namba moja ulifurika wafuasi, ndugu na marafiki wa walalamikaji hao kusubiri hatima ya kutenguliwa au kuendelea kukaa mahabusu vigogo hao.

Saa 7:00 Jaji Rumanyika aliingia katika ukumbi huo wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam kuwasomea walalamikaji hukumu ya rufani yao iliyosajiliwa Novemba 27, mwaka jana wakipinga Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwafutia dhamana kwamba walikiuka masharti yake.

Walalamikaji wamekaa mahabusu tangu Novemba 23, 2018, siku ilipofutwa dhamana yao mpaka jana, ikiwa ni siku 97 baada ya rufani hiyo kufunguliwa chini ya kiapo cha dharura.

**UAMUZI WA JAJI**

Akisoma uamuzi juu ya rufani hiyo, Jaji Rumanyika alisema dhamana ni mkataba wa pande tatu tofauti ambazo ni mahakama, mshtakiwa au washtakiwa na mdhamini au wadhamini.

Alisema pale mshtakiwa anaposhindwa kufika mahakamani na mdhamini akashindwa kueleza sababu na kwa nini fungu lake la dhamana lisichukuliwe, dhamana ya mshtakiwa inafutwa.

Kwa mujibu wa Jaji Rumanyika, matakwa ya sheria dhamana inatakiwa kuondolewa pale tu fungu la dhamana la mdhamini linaposhindwa kuchukuliwa.

Alisema katika mwenendo wa Mahakama ya Kisutu, haionyeshi wadhamini hawakuwahi kutoa maelezo kwa nini fungu lao la dhamana lisitolewe.

"Kuhusu rufani hii, uamuzi wa Mahakama ya Kisutu si tu haukuwa sahihi bali wakati wake ulikuwa haujafikia na kama mtoto kuzaliwa basi ni njiti," alisema Jaji na kuongeza:

"Hakimu Mkazi Mkuu (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu Tanzania) Wilbard Mashauri katika uamuzi wake aliegemea kwenye viapo wakati walalamikaji hawakupewa muda wa kujibu viapo kinzani. Uamuzi huo ulisababisha kufutwa dhamana hiyo," alisema jaji.

"Kufutwa dhamana hakukupaswa kufanyika katika hatua hiyo. Rufani hii ni mpya tangu nianze kusikiliza rufani mbalimbali. Imenistaajabisha kuliko zote nilizowahi kuziona," alisema kwa msisitizo.

Alisema mahakama ya chini inatakiwa kufahamu inachangia vipi msongamano wa mahabusu katika magereza nchini na kwamba izingatie uhuru wa mshtakiwa hauna mbadala.

Aidha, alisema mamlaka za maofisa wa mahakama, majaji na mahakimu za kuamua masuala ya mshtakiwa ziko kisheria.

"Mahakama ya Kisutu iliweka rehani masharti ya dhamana kwa kuwataka washtakiwa kuripoti kwa Kamanda wa Polisi Mkoa (RPC) wa Ilala, lakini katika mwenendo wake haionyeshi mahali kiongozi huyo wa polisi alitoa taarifa ya mahudhurio ya walalamikaji kwa kuwa walitakiwa kuripoti mahakamani na si vinginevyo," alisema.

"Mahakama yangu inaelekeza kwamba kuanzia sasa mnatakiwa kuripoti Mahakama ya Kisutu kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi na hamruhusiwi kusafiri nje ya nchi bila kibali cha mahakama hiyo. Walalamikaji waachiwe huru kwa dhamana na jalada la kesi ya jinai namba 112/2018 lirejeshwe katika mahakama hiyo lianze kusikilizwa mara moja," alisema Jaji Rumanyika.

Aidha, alisema kwa maoni yake majaji na mahakimu wanapaswa kuzingatia tisa katika kutoa dhamana. Alivitaja vipengele hivyo

INAENDELEA UK. 26



Rais wa Rwanda, Paul Kagame, akifurahia zawadi ya picha ya Mlima Kilimanjaro baada ya kupewa na mwenyeji wake Rais Dk. John Pombe Magufuli, baada ya mazungumzo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## JPM, Kagame wateta Ikulu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, jana aliwasili nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili na kupokewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi.

Kagame aliwasili jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, saa 9:34 alasiri akiwa ameongozana na wasaidizi wake.

Baada ya kuwasili, Kagame alifanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Ziara ya jana ya Kagame ilikuwa ya pili nchini kwa mwaka huu baada ya kufanya kwa mara ya kwanza Januari 14, mwaka huu, katika ziara ya siku moja.

Katika ziara yake hiyo, Rais Kagame na mwenyeji wake Rais Magufuli walifanya mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano baina ya Rwanda na Tanzania.

# Aliyosema Kibonde kuashiria kifo chake

**Na Romana Mallya**

"SISI wanadamu hatuna lolote katika ulimwengu huu. Kama si leo kesho, kama si kesho, keshokutwa. Huwezi kujua muda gani na siku gani wakati wako utafika, safari yako itakuwa imefika."

Ujumbe mfupi wa video uliorushwa na watu wengi kwenye mitandao ya Facebook, WhatsApp na Instagram juu ya maneno aliyoyasema mtangazaji maarufu wa Clouds Media Group, Ephraim Kibonde.

Kibonde alisema maneno hayo alipohojiwa kuhusu kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi wa Vipindi na Uzalishaji wa Clouds Media Group, Ruge Mutahaba.

Kutokana na maneno hayo na mazingira halisi yaliyopo sasa, inaonyesha kama Kibonde aliashiria kifo chake kwa kuwa ni takriban siku nne amefariki dunia tangu kuzikwa kwa Ruge nyumbani kwao Kizuru, Bukoba mkoani Kagera.

Wakati wa msiba wa Ruge, Kibonde alikuwa mshereheshaji tangu Dar es Salaam hadi Bukoba mkoani Kagera. Kwa hakika ni msiba juu ya msiba na ni pigo kwa Clouds Media na tasnia ya habari kwa ujumla kuondokewa na watu wawili chini ya wiki mbili.

Kibonde alifariki dunia alfajiri ya kuamkia jana jijini Mwanza kwa tatizo la shinikizo la damu wakati akiwahishwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando kutoka Hospitali ya Uhuru jijini humo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Clouds Media Group, Joseph Kusaga, alisema familia ya Clouds imepata pigo lingine kubwa kwa kuondokewa na mfanyakazi wao Kibonde.

Alisema Kibonde alianza kuugua akiwa kwenye msiba wa Ruge na baada ya kuanza kwa matatizo hayo, walifanya jitihada za kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera ya Bukoba kwa matibabu.

"Baada ya kupelekwa hospitali ya Bukoba ilionekana kuna umuhimu wa kumpeleka Hospitali ya Uhuru iliyoko Mwanza na alifikishwa kwenye hospitali hiyo na kupata matibabu yaliyompa nafuu. Wakati akijiandaa kurudi Dar es Salaam, hali ikabadilika ghafla na kupelekwa Bugando na hatimaye kufariki dunia. Taratibu za mazishi zitafanyika nyumbani kwake, Mbezi (Dar es Salaam)," alisema.

Wakati wa mazishi ya Ruge, mtangazaji Kibonde alikuwa miongoni mwa waliokuwa wakitangaza matangazo ya moja kwa moja kutoka kijiji cha Kizuru akionekana mzima wa afya.

Katika shughuli hiyo, Kibonde alikuwa akiongoza makundi mbalimbali yaliyojitokeza siku hiyo kwa kuyataja kwenda kuweka udongo na mashada ya maua kaburini.

Jana asubuhi, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, alithibitisha kuwa Kibonde amefariki dunia na kwamba alianza kusumbuliwa na shinikizo la damu alipokuwa Bukoba kwenye msiba wa Ruge na baadaye alihamishiwa jijini Mwanza.

Kibonde ambaye ni mmoja wa watangazaji wa kipindi cha Jahazi cha Clouds FM kinachorushwa hewani kila siku jioni, akiwa na mwenzake Gadna G Habash, alijipatia umaarufu kutokana na ucheshi wake na maneno yaliyojaa vichekesho na vitimbi.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Ofisa Muuguzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Joyce Kaiza, akimpima presha mkazi wa jiji, wakati taasisi hiyo, kupitia wataalamu wake wanawake, ilipofanya upimaji wa viashiria vya magonjwa ya moyo na kutoa elimu ya magonjwa hayo kwa wanawake, katika soko la Feri, jijini Dar es Salaam jana, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JOHN BADI**

# Askari JWTZ anaswa tukio la ujambazi

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, linamshikilia askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Friday Kumingi (29), kwa kushirikiana na majambazi kufanya matukio ya uhalifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema askari huyo alikamatwa kwenye msako uliofanywa na jeshi hilo Machi 3, mwaka huu.

Alisema askari huyo wa JWTZ Kikosi cha 36KJ Kibaha Msangani, alipohojiwa na polisi baada ya kukamatwa alikiri kumiliki silaha mbili kinyume cha sheria.

Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo aliwajulisha askari hao kuwa huwa anazihifadhi silaha hizo nyumbani kwa mke wake mdogo mtaa wa Muheza Kibaha, Pwani na huzitumia kufanyia matukio ya uhalifu katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na Pwani.

Alisema baada ya mahojiano, askari hao na mtuhumiwa walifika kwenye nyumba hiyo na kufanikiwa kukamata silaha aina ya AK 47 yenye namba NM174844 ikiwa na risasi 20.

Mambosasa alisema askari walikuta boksi moja likiwa na risasi 27, bastola moja yenye namba 3249 ikiwa na risasi saba ndani ya magazine na risasi tatu za silaha aina ya G3.

Aidha, Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo alikubali kuwaonyesha wenzake watatu anaoshirikiana nao katika matukio hayo na askari walipofika kwenye nyumba wanayoishi watuhumiwa walianza kukimbia.

Aidha, Mambosasa alisema baada ya watuhumiwa hao kuanza kukimbia kupitia mlango wa nyuma, askari walianza kurusha risasi hewani kuwaamuru wasimame, lakini walikaidi.

"Walikaidi na ndipo askari walipowafyatulia risasi za miguu ambazo ziliwajeruhi na kufariki dunia wakiwa njiani kupelekwa hospitali," alisema Mambosasa bila kutaja majina ya watu hao.

# Mtuhumiwa akiri mahakamani kufanya biashara ya binadamu

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa Wilaya ya Tunduru, Fatuma Alli (35), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya, kujibu tuhuma za kujihusisha na biashara ya kuuza binadamu. Akimsomea shtaka hilo, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Bosco Kilumbe, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alifanya kosa hilo kati ya Februari 28 na Machi Mosi, mwaka huu.

Alidai kuwa katika tukio hilo, mtuhumiwa huyo alinaswa akiwa anawatorosha wanafunzi akiwamo wa kidato cha kwanza wa Shule ya Nandembo mwenye umri wa miaka 14 (jina linahifadhiwa).

Kwa mujibu wa mwendasha mashtaka, wasichana wengine ambao walikuwa wanatoroshwa na mtuhumiwa huyo ni mwenye umri wa miaka 15, wa kidato cha kwanza na wa kidato cha pili mwenye umri wa miaka 16 (wote majina yao yanahifadhiwa). Kilumbe aliendelea kufafanua kuwa kwa kufanya hivyo mtuhumiwa huyo alifanya kosa kinyume na kifungu cha sheria namba 4 (1) pamoja na kifungu namba 5 cha Sheria ya Kuzuia Biashara ya Binadamu namba 6 ya mwaka 2008.

Mtuhumiwa alikiri kufanya kosa hilo na kujitetea kuwa alifanya hivyo akiwa anatekeleza maelekezo aliyopewa na mume wake aliyemtaja kuwa ni Hamisi Kanju, ambaye alidai kuwa alimwagiza ampelekee wasichana watakao msaidia kufanya biashara ya kuuza mgahawa.

Kutokana na mtuhumiwa huyo kukiri mashtaka yake, Hakimu Janneth Kaluyenda, aliamuru kesi hiyo ianze kusikilizwa Machi 21, mwaka huu, kwa kuanza kusikiliza ushahidi wa upande wa Jamhuri.

Mtuhumiwa yuko rumande kwa kushindwa masharti ya dhamana.

# Tanzania yaongoza kuwa na simba wengi Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imetajwa kuwa nchi inayoongoza kwa kuwa na simba wengi barani Afrika.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa African Wildlife Foundation, Kaddu Sebunya, wakati akizungumza kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa wanyamapori na mazingira kwa nchi za Afrika.

Sebunya alisema kwa upande wa tembo, Tanzania inashika nafasi ya tatu kwa kuwa na tembo wengi.

"Hii inatokana na juhudi zinazofanywa na serikali kuhakikisha wanyamapori na uhifadhi wa misitu unapewa kipaumbele," alisema.

Alisema Tanzania ni mfano wa kuigwa kwa nchi zingine katika suala la uhifadhi wa misitu na utunzaji wa wanyamapori.

Sebunya aliitaja nchi ya kwanza inayoongoza kwa kuwa na tembo wengi kuwa ni Botswana ikifuatiwa na Zimbabwe.

"Kuna umuhimu wa kila nchi ya Afrika kuweka mikakati itakayosaidia maliasili zake zitunzwe na kulindwa ipasavyo," alisema.

Aidha, alisema changamoto iliyopo kwa sasa ni upungufu wa wanyamapori hasa simba na tembo kwa sababu ya kuwapo kwa majangili na uwindaji haramu.

Kutokana na hali hiyo, Sebunya alisema African Wildlife Foundation, inahamasisha kila nchi kuweka mipango ambayo itasaidia kuwafanya simba na tembo waendelee kuwapo. Alisema endapo kila nchi ikiamua kulinda wanyamapori na uhifadhi hakuna ambacho kitashindikana.

"Mfano mzuri ni Tanzania miaka ya nyuma tembo walikuwa wanauawa, lakini kwa sasa wako salama kutokana na hatua ambazo serikali imezichukua," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA.

04 - 03 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Singida**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 135 CCP / T 161 BDU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 28
Upana - mita 3.7
Kimo - mita 5.4

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Singida Kupitia Morogoro,**

gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115098602



TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kuwataarifu wateja wetu wote na umma kwa ujumla kuwa Ndugu DUNDAS B. MFURU



***DUNDAS B. MFURU***

Mwenye picha hapo juu si mwajiriwa tena wa kampuni ya **ENTERPRISE FINANCE LIMITED** kuanzia tarehe 23/02/2019 na kwamba kampuni ya **ENTERPRISE FINANCE LIMITED** haitahusika wala kutambua miamala au mikataba au jambo lolote lile **Ndugu Dundas B. Mfuru** atakalolifanya kwa kuihusisha kampuni.

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Enterprise Finance Limited**

115101602

# Osha yaagiza kampuni za usafi kuwalinda wafanyakazi

**Na Beatrice Moses**

CHAMA cha Walimu (CWT), kimesema kinafuatilia undani wa tukio linaloonekana katika video fupi kwenye mitandao ya kijamii inayomwonyesha Meya wa Jiji la Tanga, Mustapha Selleboss, anayedaiwa kumfokea Mwalimu Gladness Twazihirwa wa Shule ya Sekondari Pande Magubeni ya jijini huko kwa kuchelewa kazini.

Taarifa kwa umma iliyotolewa juzi na Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, imeelezwa kuwa chama hicho kinafuatilia tukio hilo ikiwa ni pamoja na kukutana na wahusika na baada ya kujiridhisha, kitatoa tamko.

CWT inaeleza katika taarifa hiyo kuwa bado ina imani kubwa na serikali kwa namna inavyosimamia nidhamu ya watumishi wa umma, hasa walimu kwa kufuata kanuni na taratibu zilizopo, hivyo imeshauri mambo yanayohusu nidhamu ya mwalimu yatatuliwe na mamlaka husika za nidhamu.

Katika video hiyo, anaonekana Meya Selleboss akidaiwa kumtaka Mwalimu Twazihirwa, aeleze muda aliofika kazini siku hiyo.

Katika video hiyo, sauti inayodaiwa ya Mwalimu Twazhirwa inasikika akijibu kuwa aliripoti kazini saa moja kasoro dakika ishirini na tano, majibu ambayo yanaonekana kumkera kiongozi huyo wa kisiasa

INAENDELEA UK. 8




Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kituo cha Kigamboni, Mathias Marshal, akitoa elimu juu ya kinga na tahadhari ya majanga ya moto na kuendeleza kampeni inayoitwa "mlango kwa mlango nyumba salama" iliyoanzishwa na jeshi hilo, mwaka jana, katika soko la samaki la Magogoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Ugonjwa wa kimeta wadhibitiwa

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

SERIKALI imesema mlipuko mpya wa ugonjwa wa kimeta katika wilaya za Moshi, Rombo mkoani Kilimanjaro na Longido mkoani Arusha umedhibitiwa, hivyo kuwatoa hofu wananchi wa wilaya hizo kuhusu ulaji wa nyama.

Ugonjwa huo ambao hushambulia wanyama walio na damu moto, huku kwa binadamu ukiambukizwa kwa kula nyama ya mnyama mwenye ugonjwa au aliyekufa kwa ugonjwa huo, uliripotiwa kuzuka kwenye maeneo hayo Februari 21, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Hezron Nonga, alisema wameudhibiti ugonjwa huo kwa kutoa chanjo kwa mifugo.

Alisema kurugenzi yake kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imetoa dozi 100,000 za chanjo ya kimeta kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido kukabidhiwa dozi 35,000, Moshi 40,000 na Rombo 25,000.

"Tunafikiria kuondoa karantini ya usafirishaji wa mifugo katika maeneo mbalimbali katika halmashauri kwa kuwa baada ya kuanza kwa chanjo hakuna kesi mpya za ugonjwa huo zilizojitokeza," alisema.

Aidha, Dk. Nonga alisema Halmashauri ya Wilaya ya Longido imenunua dozi 16,700

INAENDELEA UK. 8




# Kambi wazee hatarini kukumbwa na magonjwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZEE wanaolelewa kwenye kambi ya Busanda wilayani Shinyanga, wako hatarini kupatwa na mlipuko wa magonjwa kutokana na kujaa kwa choo wanachokitumia.

Choo hicho kilijengwa miaka mingi na sasa kimeshachoka na hakifai tena kwa matumizi, lakini kutokana na ukosefu wa choo, wazee hulazimika kukitumia hivyo hivyo.

Wazee walipaza kilio hicho jana, wakati maofisa wa maendeleo ya jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, kwa kushirikiana na Shirika la PAWWCO linalojishughulisha na shughuli za kijamii mkoani hapa, walipotembea kuwapatia msaada wa nguo, chumvi na sabuni za kufulia.

Mmoja wa wazee hao, Elizabeth Mhari, alisema kambi hiyo imekuwa ikikabiliwa na ubovu wa choo kwa kuwa kilichopo ni kibovu na kimeshajaa na wamekuwa wakikitumia hivyo hivyo, hali ambayo imekuwa ikihatarisha usalama wa afya zao.

"Changamoto kubwa ambayo tunakabiliana nayo hapa ni ubovu wa choo kwa kuwa kimeshajaa kabisa. Tunaomba msaada wa kutengenezewa kingine hiki hakifai kabisa kinahatarisha usalama wa afya zetu," alisema Mhari.

"Pia tunapongeza msaada ambao tumepatiwa na tunaomba watu wengine wajitokeze kuja kutusaidia ikiwamo kutuletea chakula hasa mchele ili na sisi tupate kuja kusherehekea vizuri sikukuu ya Pasaka," aliongeza.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, alisema wameamua kutembelea kambi hiyo kuwaenzi wazee katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani na kuahidi kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau wataendelea kutatua changamoto za wazee hao.

Mratibu wa PAWWCO, Madaga Joseph, alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali katika kutatua changamoto mbalimbali ndani ya jamii ikiwamo kambi hiyo ya kulea wazee.

TOLEO MAALUM

# USHIRIKIANO WA JICA KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI DAR ES SALAAM

JICA

## SEHEMU YA TATU:

## KUTOKA DARAJA LA JUU LA MFUGALE HADI DARAJA LA GEREZANI



Daraja hili la gerezani litajengwa upya kwa chuma cha pua, ili liweze kutumiwa na mabasi yaendayo haraka (BRT) na reli ya kisasa ya umeme (SGR). **PICHA: JICA**

MNAMO Januari 2019 Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mkandarasi wa Japani, Sumitomo Mitsui Construction Company (SMCC), walitiliana saini mkataba wa ujenzi wa daraja la Gerezani. Utiani saini huo ulishuhudiwa na Eng. Issack Kamwelwe, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Bwana Toshio Nagase, Mwakilishi Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA) Ofisi ya Tanzania. Ni matarajio ya JICA na Serikali ya Tanzania kwamba daraja jipya la Gerezani litachangia katika kupunguza msongomano wa magari jijini Dar es asalaam.

Ufunguzi wa Daraja la Nyerere mwaka 2016 ulibadilisha usafirishaji kutoka Kigamboni kuja katikati ya Jiji (Central Business District) lakini daraja la sasa la Gerezani lilikua kikwazo katika kupunguza msongamano wa magari. Hivyo Serikali ya Tanzania na JICA waliona tatizo hilo na kuamua kulishughulikia. Daraja jipya la Gerezani litakua ni ishara ya usafirishaji ulioboreshwa Dar es salaam kwani mabasi ya Mwendokasi yatapita sambamba na daraja hilo. Aidha Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway (SGR) itapita chini ya daraja hilo. Daraja hili jipya litarahisisha usafiri wa kwenda na kutoka Bandari ya Dar es salaam hivyo kukuza uchumi wa Tanzania. Isitoshe kwa kuwa Bandari ya Dar es salaam hushughulikia asilimia 40 ya mizigo iendayo nchi jirani kama vile Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Rwanda, mradi huu unatarijiwa kuchangia ukuaji wa uchumi wa kanda hii pia.

Jiji la Dar es salaam litakua Jiji kubwa (mega city) ifikapo miaka ya 2030 kwani linatajrajiwa kuwa na idadi ya watu inayozidi milioni 10 wakati huo. Majiji makubwa kama vile Paris, New York, Tokyo, Delhi, Shanghai n.k. yana mtandao wa usafirifishaji mzuri. Kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania mwaka 2018, JICA ilikamilisha utayarishaji wa Mpango Kabambe wa Usafirishaji Dar es salaam kwa kuzingatia ukuaji wa jiji hilo. Pamoja na uboreshaji wa usafirishaji wa mtandao wa barabara Mpango huo Kabambe umeainisha uanzishwaji wa njia mpya za usafishaji kama vile upanuzi zaidi wa shughuli za Mabasi ya Mwendo Kasi (BRT), usafiri wa reli (commuter rail) na "Intelligent Transport System" (ITS).

Miundombinu ni msingi wa nchi na watu wanaojenga miundombinu ni msingi wa taifa. Kama Mwalimu Nyerere alivyowahi kusema: "Ili kuwepo na maendelo ya kweli, lazima watu washirikishwe". Kampuni ya Kijapani iliyojenga Daraja la Mfugale (SMCC), ilitimiza lengo hilo la Mwalimu Nyerere kwani iliweza kukamilisha ujenzi wa daraja hilo bila ajali yeyote kutokea. Isitoshe wakati wa ujenzi wa Daraja hilo Kampuni hiyo pia iliwaongezea ujuzi Watanzania waliokua wanafanya kazi na katika Kampuni hiyo. Tunaamini kwamba Watanzania hao wataungana pamoja kujenga Daraja la Gerezani.

JICA ni mshirika mwaminifu wa maendeleo ya Tanzania. Tutafanya kazi pamoja na Serikali ya Tanzania pamoja na watu wake wote.

### JICA (Japan International Cooperation Agency):

**Ni Shirika la Umma la Serikali ya Japani linalosimamia misaada yote inayofadhiliwa na Serikali ya Japani (Official Development Assistance (ODA). JICA ni miongoni mwa mashirika makubwa sana duniani linalosaidia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi mbalimbali zinazoendelea. Nchini Tanzania, JICA imekua mshirika mwaminifu kwa Tanzania katika nyanja mbalimbali kwa zaidi ya miaka 50 kuanzia mwaka 1962. Katika sekta ya usafirishaji mijini ushiriki wa JICA ulianza mwaka 1980 kwa ufadhili wa ujenzi wa Daraja la Selandar jijini Dar es salaam.**

215102902

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Wanawake ni darasa tuwaige, tubadilike*

**HONGERENI** wanawake wa Tanzania kwa kuadhimisha siku yenu ambayo pamoja na kuitumia kutafakari mafanikio, changamoto na fursa, pia ni wakati wa kusherehekea ushindi.

Tunasherehekea ushindi kutokana na mambo makubwa tunayoyaona katika zama hizi, hasa nguvu kubwa iliyo katika ujasiriamali unaofanywa kila mahali na wanawake wa taifa hili.

Tunawapongeza kwa juhudi kubwa zinazoonekana kwenye kujitambua na kujiingiza katika kujifunza na kuzitumia mbinu za utafutaji na uwekezaji mdogo na mkubwa karibu kila mahali katika nchi yetu. Hongereni wanawake. Mmejiongeza na kuonyesha tofauti na ilivyokuwa hapo zamani. Wanawake si watu wa kulala nyumbani na kusubiri kuhudumiwa na wenza wao.

Tunaweza kusema zama hizi zimebadilika idadi ya wanaume wanaokaa vijiweni ni kubwa kuliko ilivyokuwa hapo zamani.

Mathalani, jijini Dar es Salaam, ukiangalia pembeni ya barabara au kwenye vituo vya mabasi bila hata kuingia mitaani unaweza kupata takwimu za kutosha kuthibitisha ukweli huo.

Ni dhahiri kiwango cha uzalishaji kwa upande wa kinababa kimeshuka na kuna changamoto kuwa wengi wanashinda na kuishia kujibanza vijiweni, maskani na kwenye mabaraza ya kahawa. Haya yanaonekana kila mahali, anapotokea fundi viatu mmoja kijiwe chake kinajaa wanaume wanaofika kupiga soga na kupoteza wakati hadi anapofunga jioni au usiku.

Hali ni hiyo hiyo kwa mafundi baiskeli na pikipiki chini ya mwembe, vinyozi, wajaza upepo kwenye matairi na wauza kahawa na kashata. Ni vivyo hivyo, kwenye baa zenye wachezaji 'pool'. Maeneo hayo japo anayehusika na kazi ni mmoja au wawili katika kundi la wanaume wazee kwa vijana wanaomzunguka ni kubwa kuliko maelezo.

Vijana hao hukaa kijiweni bila kazi wala mipango kwa muda wote. Wanaamkia na kushinda huko bila kujali kuwa mchango wao kwenye familia unahitajika na asiyefanyakazi si vyema akala.

Wanawake sivyo, si wakaaji vijiweni wakati kinababa na vijana wanapoteza muda kusogoa na kudanganyana, kinamama ni wajasiriamali mitaani. Wanasuka nywele, kupika na kupakua lakini pia hupaa angani kwenda ng'ambo kununua bidhaa za madukani. Ni ukweli kuwa wakati wanaume wanapanga cha kuongea vijiweni, barazani na kwenye maskani wanawake wanakimbia baharini, ziwani na mitoni kununua samaki kuwaandaa na kuuuza.

Wapo wanaokwenda sokoni kusaka bidhaa za magengeni na madukani. Kuna wanaouzungusha bidhaa hizo mitaani wakitembea nyumba kwa nyumba kuuza na kuchukua chao mapema.

Tunawapongeza wanawake kwa uthubutu, ujasiriamali, ubunifu na kuibua mbinu mpya za utafutaji. Hatua hiyo, tunaiona kama uzalendo wa dhati wa kukuza uchumi wao binafsi, wa familia zao na taifa pia. Tunawahamasisha kuwa jinsi mnavyojiimarisha kiuchumi, ndivyo ambavyo mnakuwa imara katika masuala ya uongozi na kupaza sauti zenu katika kuongoza na kusimamia maendeleo ya taifa kwa kuwa viongozi.

Haitoshi kumiliki uchumi pekee, bali jitihada mlizozionyesha kwenye uzalishaji na ujasiriamali zitumike kwenye kuongeza ushawishi wa uongozi wa umma na kuwa sehemu ya viongozi wa taifa ili mshiriki kwenye uongozi wa nchi.

Tunawashauri wanaume kujifunza kwa wanawake na kushirikiana nao kuendeleza jitihada wanazozionyesha kwenye ujasiriamali na uwekezaji. Washirikiane nao ili wawe viongozi wa vitongoji, serikali za mitaa, mabaraza ya kata, madiwani na ndani ya bungeni ili msimamie maendeleo ya nchi.

Haitoshi kuridhika kuwa mnaua na kununua, mnamiliki mali na fursa mbalimbali pamoja na nguvu za kiuchumi bila kuonyesha makeke na uwezo wenu kwenye kuongoza taifa. Jitihada hizo zianzie kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Siku ya Wanawake itapendeza kwa kupinga ukatili kivitendo*

**VITENDO** vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, vikiwamo kutopandishwa vyeo, kutolipwa maslahi na ujira mdogo, kutoajiriwa na kuombwa rushwa ya ngono ili wapate haki zao, ni changamoto inayowakabili wanawake.

Mbali na hivyo, vitendo vingine ni kupoteza ajira pale wanapojifungua, kunyimwa kinga na likizo za uzazi, hata ruksa ya kunyonyesha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ndiye anaamua kukemea hayo, kwamba ni dhana ya kibaguzi na haikubaliki.

Anaeleza kwamba, zina madhara makubwa kwa wanawake, kwa sababu vinawanyima fursa sawa katika ajira, hivyo kusababisha watumbukie katika lindi la umaskini na kuathiri mchango wao katika ukuzaji uchumi wa nchi.

Waziri Mhagama, alitamka hayo mwaka juzi, alipofungua kikao cha viongozi wanawake wa vyama vya wafanyakazi nchini wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) jijini Dodoma. Hapo ndipo, alipovitaja vitendo vya ukatili, ambavyo wanawake wanakumbana navyo.

"Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Namba 6 ya 2004, inaeleza ni marufuku kwa mwajiri kumbagua mfanyakazi katika masuala yahusuyo kazi na ajira, kwa misingi ya jinsia, ujauzito na majukumu ya kifamilia," anasema Mhagama.

Anasema nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ikiwamo Tanzania, zilipitisha ajenda ya Maendeleo Endelevu 2030 yenye malengo 17. Miongoni mwake ni lengo namba tano linalohusu usawa wa kijinsia katika nyanja zote za kiuchumi na kijamii.

Pamoja na vitendo hivyo, bado kumekuwapo na changamoto kadhaa zinazowakumba wanawake, zikiwamo hizo anazotaja Waziri Mhagama, ambazo kimsingi zinahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Leo ni tunaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Tanzania ikuungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku hiyo, kupitia kaulimbiu: "Badili Fikra Kufikia Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu."

Ni siku inayoadhimishwa kila Machi 8 ya mwaka, ikiwa na kaulimbiu za mwaka zinazolenga kuhamasisha jamii kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na kuzingatia usawa wa kijinsia.

Historia inaonyesha kuwa zaidi ya karne sasa imepita, umma unaadhimisha siku hiyo, lakini bado wanawake wameendelea kukumbana na changamoto zinazochangia kuwafanya waonekane ni wanyonge.

Siku ya Wanawake Duniani, inatathmini maendeleo ya wanawake katika jamii kwa namna mbalimbali, ikiwamo kiuchumi inalenga kuondoa mfumo dume, ambao umewafanya wanyanyasike.

Serikali nchini imeshaweka wazi kwamba imeandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, kwa lengo la kupunguza kiwango cha ukatili kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Inasema kwamba, mpango huo ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia (2005); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana - (1998).

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alikaririwa akisema hayo Desemba mwaka jana, alipozindua kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. Alisema serikali imeandaa mpango huo kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika ngazi ya makundi ya jamii za kitanzania, kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Anautafsiri ukatili wa kijinsia, ni utendaji wa maovu, na vinavyodhalilisha, kutesa, kunyanyasa, kukandamiza, visivyojali haki za kuishi kwa binadamu yeyote, awe wa kike au wa kiume.

Majaliwa anasema, ukatili wa kijinsia huja katika taswira nyingi, kuanzia vipigo, ubakaji, ukeketaji, ulawiti, matusi, lugha na vitendo vya udhalilishaji, pia kunyimwa fursa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

"Hivyo, ukatili wa kijinsia ni unyanyasaji wowote unaofanywa na mtu dhidi ya mwingine, bila ya kujali umri, maumbile, kabila, rangi, dini au mtazamo wa kisiasa.

"Unyanyasaji huu unahusisha mambo mengi kama kumpiga mwanamke au mwanaume, kumnyima mtoto elimu, kumlawiti mtoto wa kike au kiume, kumbagua mtu katika mahitaji ya msingi au kuwanyima urithi warithi wanaohusika," anasema Majaliwa.

Hivyo, Tanzania inapoungana na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Mataifa kuadhimisha siku hiyo, ni vyema suala la kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanawake lizidi kutiliwa mkazo.

BARUA/MJADALA

## *Tuwarekebishe vijana mila*

**Mhariri,**

*HIVI sasa ndani ya jamii kuanzia shuleni hadi nje ya shule kuna mijadala ya kina kuhusu mazingira ya watoto wa kizazi hiki kuwa mbali na utamaduni wao.*

*Wanaelezwa sasa, wako zaidi katika utamaduni unaoendana na yanayojitokeza katika mazingira na teknolojia mpya, inayotawala sasa.*

*Wazazi na walezi tumekuwa wakali na walalamishi kuhusiana na mabadiliko hayo ya kiutamaduni na mila.*

*Sijui ni watoto wangapi leo wanaojua michezo kama goroli, 'tiyari bado' na mingine mingi katika jamii zao. Haishangazi kukuta kundi la watoto hao, wanahesabika.*

*Kama mtazamo ni huo kuna haja ya kujiuliza zaidi, nini sababu za msingi? Hapana shaka ni mabadiliko kwamba, mifumo ya mawasiliano imekamata maisha yao.*

*Namna ilivyokamata ni inawahamasisha kutawaliwa na hayo ambayo ni matokeo ya teknolojia kwa jumla, kukiwapo mabadiliko makubwa katika teknolojia ya mawasilianio ya umma.*


*Hivyo, sisi tulio na umri ambao umeshuhudia vipindi tofauti vya ukuaji, kabla ya teknolojia na baada ya hapo, tuna mengi ya kueleza na tunawajibika nayo, katika sura ya ukubwa na wajibu wa ulezi.*

*Tunapaswa kukifanya hicho katika mtazamo wa uazi kwa maana ya tunawajibika kusimamia mwelekeo kiimani na kimaadili, pia katika elimu ya wanachopaswa kukifahamu kimaadili.*

*Hivyo, tusiishie katika kuwalaumu 'kwa nini wamekuwa hivi' bali kuwatengenezea mwelekeo.*

**Abbas H. Abbas,**
**Pangawe, Morogoro.**

# Ukikomboa fikra za mwanamke, umeshaikomboa jamii yako




**Na Salome Kitomari**

**BARAZA** la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), limesema asilimia 70 ya wanawake wajasiriamali Tanzania wamewezeshwa kupata mikopo ya kukuza biashara, ambazo zimeajiri mamia ya Watanzania.

Katibu wa NEEC, Beng'I Issa, anasema kwenye eneo la mikopo, wanawake wanafanya vizuri kwa kuwa mwaka 2015 asilimia 36 ilikuwa inaenda kwa wanawake, lakini baada ya elimu sasa imefikia asilimia 70.

"Wajasiriamali wengi Tanzania ni zaidi ya milioni tatu, ambao asilimia 57 ni wanawake ambao wanachukua mikopo na kuirejesha kwa wakati, ikiwamo kutumia fedha wanazopata kwa ajili ya maendeleo ya familia, ikiwamo kujenga makazi na kusomesha watoto," anasema Issa.

Anasema, changamoto kubwa kwa wakopaji wengi ni kukosa uaminifu kwa kuwa baada ya kupewa fedha hubadili namba za simu na makazi, kumkwepa aliyemkopesha, jambo linalowafanya washindwe kuaminiwa na taasisi za fedha.

"Ukichukua vijana 100, ukasema unataka kuwawezesha ufike nao mahali fulani baada ya muda utabaki na vijana watatu. Vijana wajue biashara ni uaminifu na ndiko mafanikio yaliko na uaminifu wakati mwingine ni mtaji, suala la uaminifu kwenye biashara ni muhimu sana," anasema Issa.

Kwa mujibu wa Issa, baraza linapokea vijana wengi wanaolilia kukosa mtaji, lakini wanapopewa au kukutanishwa na taasisi za fedha na kukopeshwa, wengi hubadilika na kupotea, jambo linalowakwamisha wasinufaike na mikopo hiyo.

Issa anasema, kuna vijana waliojaliwa kuwa na kipawa cha kuendeleza wazo linaloajiri watu wengi na kuchangia maendeleo ya Taifa, badala ya kuishi kwa kutegemea ajira pekee, ambayo inakuwezesha kupata mshahara pekee.

"Tusipoteze muda kutafuta kazi kwa muda mrefu, wakati unatafuta kazi na una kitu unaweza kufanya ni vyema ukafanya na kupata kipato na kuondoa akili kwenye kusubiri kuajiriwa pakee," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa mapendekezo ya sasa ni ujasiriamali ufundishwe kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu, na kwamba wamekutana na taasisi zinazotengeneza mitaala ambayo inatumika shuleni na vyuoni.

"Imepita miaka minne toka mtaala uanze. Tunaona mafanikio ni kwamba vyuo vingi vimekuwa na programu za ujasiriamali na shule zinafundisha, japokuwa siyo kwa kiwango kilichotarajiwa. Pia, tuna programu ya vijana nje ya shule waliomaliza chuo kikuu na wanafikiria kufanya biashara," anasema.

Anasema: "Tunawafundisha mafunzo mbalimbali ikiwamo jinsi ya kuandika andiko, tunamsikiliza tunaboresha wazo lake, lakini baada ya kumkutanisha na taasisi za fedha, masoko na ushirika, nia ni kuuza wazo lake ili aweze kupata ufadhili."

Issa anasema kwamba, mawazo hayo huangalia sekta za kilimo, mifuko na mazingira na baada ya mchakato, hupelekwa mbele ya majaji wanaoamua washindi watatu wa mwanzo na wanapewa mtaji wa kuendesha biashara na wengine huunganishwa na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo.

Katibu huyo anasema, baraza lina programu ya kuwatembelea vijana mbalimbali zaidi ya 2,000 ambao wamejiajiri na kuajiri Watanzania wengine na wameaminiwa na taasisi za fedha.

Anasema kuwa barani Afrika, Tanzania imeshapiga hatua kubwa katika huduma za simu za mkononi, ikiwa yanaingiliana na huduma za fedha na sasa Watanzania wengi wana huduma ya simu za mkononi.

Issa anaeleza kuwa, utafiti wa hivi karibuni umebaini kuwa asilimia 65 ya Watanzania, wanatumia huduma za fedha kwenye biashara zao, kwa kuwa wapo ambao hawana akaunti, lakini wanafanya manunuzi na matumizi.

KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Osha yaagiza kampuni za usafi

INATOKA UK. 4

ambaye aliendelea kuhoji zaidi kuhusu muda wa kuripoti kazini kwa mwalimu huyo.

"Hivi mfano, angekuwa ni ofisa elimu amekuja hapa, mngeleta sababu hizo, au angekuja Waziri wa Elimu mngeleta sababu hizi? Waziri wa Elimu na mimi ni sawasawa, yeye ni mwanasiasa na mimi ni mwanasiasa, yeye ni uteuzi tu wa mkuu wa nchi," inasikika sauti inayodaiwa kuwa ya meya huyo katika video hiyo. "Sikia vizuri, mimi ndiyo mwenye halmashauri, naweza kukwambia sikutaki kwenye jiji hili na ukahamishwa kwenye shule nyingine," sauti inayodaiwa ya Meya Selleboss inasikika katika video hiyo.

Nipashe ilimtafuta Meya Seleboss kujua ukweli wa kinachoonekana kwenye video hiyo na alikiri kuwa video hiyo ni sehemu ndogo ya kilichojitokeza wakati wa ziara yake ya pili yenye lengo la kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha nne jijini mwake.Alisema ziara ya kwanza aliifanya mwaka jana huku akibainisha kuwa, mbali na kuanzisha vita dhidi ya ufaulu duni, pia wanapambana na changamoto ya kukatishwa masomo kwa wanafunzi kutokana na mimba, akieleza kuwa wanafunzi sita hadi 10 hukumbwa nayo kila mwaka.

Alidai alibaini mwalimu aliyekuwa akimuhoji, alisaini kwenye daftari la mahudhurio kwamba aliripoti kazini saa 12:38 asubuhi tofauti na alivyojibu wakati alipomuuliza.

**KAULI YA JAFO**

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alilitumia tukio hilo kuwataka viongozi wa kisiasa kuwaheshimu watumishi wa umma na kuacha kuwadhalililisha hadharani.

Alisema udhalilishaji wa watumishi wa umma ambao umekuwa ukifanywa na baadhi ya viongozi hao, ni kinyume cha maadili ya utumishi wa umma na umekuwa ukichangia kushusha ari ya utendaji wa watumishi husika.



Mwendesha guta akiwa amebeba matenga matupu na abiria, katika eneo la Feri jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Ugonjwa wa kimeta wadhibitiwa

INATOKA UK. 4

za chanjo ya kimeta, huku Moshi ikinunua dozi 30,600.

Kutokana na dozi hizo, alisema jumla ya ng'ombe, mbuzi na kondoo 18,388 wamechanjwa katika wilaya hizo zenye jumla ya mifugo hiyo 1,507,265. Longido imechanja mifugo 10,025, Moshi 8,051 na Rombo 302.

Akitoa ufafanuzi wa matukio ya ugonjwa huo, Dk. Nonga alisema hadi Machi 5, mwaka huu, katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ng'ombe wanne, mbuzi wawili na nguruwe mmoja walikufa huku Longido wakifa twiga mmoja na ng'ombe mmoja.

Aidha, Dk. Nonga alikanusha taarifa za kuwapo kwa idadi kubwa ya watu waliougua kimeta na kusema kilichofanyika ni kutoa dawa za kujikinga kwa wote ambao walikuwa jirani na mifugo iliyokufa.

Pia aliwataka wafugaji wote kuhakikisha wanachanja mifugo yao kila mwaka na kwamba mfugaji yeyote atakayekwepa kufanya hivyo, atakabiliwa na adhabu ya faini ya Sh. 500,000 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote mbili.

"Hizi dawa za chanjo zinauzwa kwa bei ya chini sana kwa kuwa zina ruzuku. Dozi moja haizidi Sh. 200 na lengo letu ni kuhakikisha bei inashuka zaidi hata ikiwezekana kuuzwa kwa Sh. 50," alisema.

# Aliyosema Kibonde kuashiria kifo chake

INATOKA UK. 2

**WENGI WAMLILIA**

Tangu kutangazwa kwa taarifa za msiba huo jana asubuhi, watu mbalimbali walianza kueleza wanavyomfahamu Kibonde huku wakikumbushia msiba wa Ruge na ule wa mke wake, Sarah, uliotokea mwaka jana.

Katika mtandao wa Instagram moja ya picha iliyotumiwa na watu wengi ni ambayo inamwonyesha Kibonde akimhoji Ruge wakati huo wakiwa vijana.

Kabla ya kumzika Ruge, mtangazaji huyo aliweka picha ya mke wake marehemu Sara Kibonde kwenye ukurasa wake wa Instagram. Watu wengi walichangia kwa kumpa pole ya 'RIP Sarah'.

Baadhi ya watu walioguswa na msiba huo ni pamoja na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ambaye katika ukurasa wake wa Instagram, aliandika: "Poleni sana Clouds kwa pigo hili kubwa! Hakika mnapitia katika kipindi cha majaribu.

"Mungu awatie nguvu. Njia yetu ni moja...pole nyingi kwa familia, ndugu na marafiki wa marehemu. Tunamwombea pumziko la amani ndugu yetu Ephraim Kibonde."

Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Harrison Mwakyembe aliandika Instagram maneno yanayosomeka hivi: "Taarifa za kifo cha mtangazaji mahiri na maarufu nchini, Kibonde wa Clouds, zimenishtua sana. Ni pigo la pili kubwa kutokea katika kipindi kifupi. Si tu kwa Clouds Media bali kwa tasnia nzima ya habari."

Aliendelea kuandika: "Wakati tunasubiri kutoka kwa madaktari kujua chanzo cha kifo chake na vilevile mipango ya mazishi yake, nitumie nafasi hii kuipa pole familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki, wana Clouds Media na wana habari wote kwa ujumla, kwa msiba huu mkubwa. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe."

**JK ATOA YA MOYONI**

Naye Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, aliandika kwenye Twitter akisema: "Majonzi yangali nasi, nimepokea taarifa ya kifo cha mtangazaji Ephraim Kibonde wa Clouds. Ni pigo kubwa kwetu sisi wapenzi wa kipindi cha Jahazi."

Kikwete, maarufu kama JK, aliendelea kuandika: "Jahazi litaeleaje bila ya nahodha Kibonde? Mwenyezi Mungu na aipe faraja familia yake, Clouds na wasikilizaji wote wa Jahazi." Mfanyabiashara maarufu, Mohamed 'MO' Dewji, katika ukurasa wake wa Instagram aliandika: "Nawawaza watoto wake, wamebaki yatima, Mungu awape nguvu. Pumzika kwa amani Kibonde, Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un."

Msanii wa bongo Fleva, Judith Wambura, 'Lady J Dee' naye aliandika Instagram, "Hili ni jambo zito kwa watu wenye ukaribu na Ephraim Kibonde. Tunakaa tunakunywa, tunacheka siku nyingine mmoja wetu anatwaliwa."

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, aliandika kwenye Intagram: "Hakika inatosha kifo kuwa ni mawaidha tosha kwa wanadamu. Kama mpenzi wa kipindi cha Jahazi la Clouds, tutammiss sana 'brother' Kibonde kwa ucheshi, umahiri na kipaji chake cha pekee. Poleni familia na Clouds Media Group."



# Unywaji wa dawa za kienyeji chanzo kifo wajawazito

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

UNYWAJI wa dawa za kienyeji wajawazito umeelezwa kuwa ni miongoni mwa kisababishi cha kutokwa damu nyingi kabla, wakati na baada ya kujifungua na kusababisha vifo vya uzazi.

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Programu (Mradi) ya Afya ya Uzazi Salama (MOHCDGEC), kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Martha Shakinyau, katika mkutano na wadau wa afya wa kutambulisha Jukwaa la Naweza, Kanda ya Ziwa na Magharibi, uliofanyika jijini hapa.

Alisema sababu moja wapo ya mama kutokwa damu nyingi kabla, wakati na baada ya kujifungua ni pamoja na unywaji wa dawa nyingi za asili kwa mjamzito ambao unasababishwa na mila na desturi potofu kwa baadhi ya makabila nchini ya kunywa dawa wakati wote wa ujauzito.

Alisema, kinamama 556 hupoteza maisha kwa kila vizazi hai 100,000 kila mwaka sawa na wanawake 11,000 kwa mwaka, 916 kwa mwezi, 211 kwa wiki, 30 kwa siku na takribani mwanamke moja kwa saa na vinavyosababishwa na kutokwa na damu nyingi kabla, wakati na baada ya kujifungua ikiwa ni asilimia 28 na vifo vingi vya uzazi hutokea Kanda ya Ziwa.

Shakinyau alisema, Wizara ya Afya inashauri wajawazito kutokunywa kitu chochote kinachoitwa dawa ikiwamo za asili bila kupata ushauri wa daktari kwa kuwa zinaweza kumletea matokeo mabaya ya kiafya na kwa mtoto.

Alisema, malengo ya taifa katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi ni kupunguza vifo kutoka 556 hadi 292 kwa vizazi hai 100,000 ifikapo 2020, ili kufikia hayo inapaswa kila mmoja kuhakikisha anawajibika na kumwelimisha mjamzito kuhudhuria kliniki mapema, kufika katika vituo vya afya wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

Meneja Kanda wa Mradi wa Fhi360 USAID Tulonge Afya, Frank Rweikiza, alisema wameanzisha jukwaa la Naweza maalum kwa mawasiliano ya afya kwa watu wazima linalolenga kuleta mabadiliko chanya ya tabia kwa jamii chini ya Wizara ya Afya na kuwezeshwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), kupitia mradi wa USAID Tulonge Afya, litakalosaidia mjamzito kupata taarifa sahihi ya namna ya kuhudhuria kliniki, kwenda vituo vya afya wakati na baada ya kujifungua, kujikinga malaria yeye na mtoto chini ya miaka mitano pamoja na kuanza kutumia vidonge vya kuf ubaza makali ya VVU ili kumkinga mtoto na maambukizi kwa atakayebainika ameathirika.

Ofisa Mradi (Programu) wa Mawasiliano ya Afya, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma kutoka Wizara ya Afya, Dk. Tumaini Haonga, alisema wanataka ifikie kila mmoja anaweza kuhakikisha vifo vya mama na mtoto chini ya umri wa miaka mitano kutokana na malaria vinapungua.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Emily Kasigara, alisema watu wengi hawana elimu ya kwenda kwenye vituo vya afya, hivyo kupitia jukwaa hilo litumike kuwaelimisha na wafike hadi vijijini pamoja na kuendelea kuhamasisha jamii kuachana na mila potofu ya unywaji dawa ovyo hasa za asili kwa wajawazito.

Naye Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Wilaya ya Nyamagana, Bertha Yohana, alisema, kinamama wengi wanatumia dawa nyingi za asili wanapokuwa wajawazito hivyo kusababisha kutoka damu nyingi wakati wa kujifungua, pia aliomba serikali kuboresha hospitali za mikoa iweze kumpokea mama wakati anapopata dharura ili kuokoa maisha ya mama na mtoto na siyo kutegemea Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (kushoto), akiteta jambo na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche (kulia), wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji cha Nyamongo, wilayani Tarime, Mkoa wa Mara juzi. **PICHA: WM**

# TFS kuweka viwango ubora mazao ya misitu

**Na George Tarimo,** MUFINDI

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS), imeanzisha mkakati wa kuweka viwango vya ubora wa mazao ya misitu ili kuondoa changamoto kwa wateja wao kununua bidhaa zisizo na ubora.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa shamba la miti la Sao Hill lililopo wilayani Mufindi, Helbert Haule, kuwa tayari watafiti wa ubora wa mazao ya misitu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), cha mkoani Morogoro wanaendelea na mchakato huo ili kuwezesha mazao ya misitu kupata nembo ya uthibitisho kutoka kwa wakala wa viwango (TBS). Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuondoa malalamiko ya bidhaa zisizo na ubora zinazoingia sokoni kutokana na baadhi ya wakulima binafsi kuvuna mazao yao kabla ya kukomaa hali inayowawia vigumu wateja kutofautisha viwango vya ubora wakati wa manunuzi. Pamoja na kufanya hivyo ni kutokana na wimbi kubwa la wakulima binafsi kuvuna mazao ya miti ambayo hayajakomaa na kuibua changamoto ya utambuzi wa ubora kwa wateja. Haule aliwataka wananchi wanaozunguka mashamba hayo kulinda miti iliyopandwa, huku akibainisha kuwa TFS itaendelea kubuni shughuli mbadala zitakazowasaidia wakulima kuwa na kipato kitakachokidhi mahitaji yao ili waweze kujiepusha na uvunaji wa miti kabla ya kukomaa.

Alisema kuwa changamoto wanazokabiliana nazo katika usimamizi wa rasilimali hiyo muhimu kwa uhifadhi na upatikanaji wa malighafi zitokanazo na miti ni mgogoro wa mipaka baina ya wananchi wanaozunguka shamba hilo pamoja Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na kuongeza kuwa wakala hao wanaendelea kulishughulikia ili liweze kutatuliwa.

Naye Switbert Kalinga ambaye ni mmoja wa wavunaji wa miti katika shamba la miti la Sao Hill alisema kuwa shamba hilo limewanufaisha kwa kiasi kikubwa kwa wengine kujiajiri baada ya kupata mitaji baada ya kuvuna. Kalinga alisema kuwa changamoto kubwa wanayopata wavunaji wa misitu ni bei ya magogo ambayo ni kubwa ikilinganishwa na uuzwaji wa magogo ambao upo chini, huku ikileta athari kubwa kwa walaji wa zao hilo.

# Mbunge atoa tani 7 za saruji kuchangia ujenzi mabweni

**Na Steven William,**
MUHEZA

ZAIDI ya tani saba za saruji zimetolewa na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi Rajabu, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma katika Shule ya Msingi Mbaramo, wilayani Muheza mkoani Tanga. Msaada huo utaongeza nguvu kwenye ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi hao wenye uhitaji maalum (wenye tatizo la usikivu) ili waweze kukaa shuleni.

Akizungumza kwa niaba ya mbunge huyo Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Mohamed Moyo, katika harambee ya kuchangia ujenzi wa mabweni hayo, alisema kama wataandaa kambi ya vijana ama wanawake kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mabweni hayo, atasaidia kuwalisha wakiwa kambini hapo kwa kuwanunulia chakula na vifaa. Mbunge wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi, pia alisema serikali inatekeleza miradi minne ya maji wilayani Muheza kwa lengo la kumaliza kero ya tatizo la maji kwa wananchi wa Muheza wanaoishi vijijini na mjini.

Balozi Adadi Rajabu alisema kuwa anawahakikishia wananchi katika Wilaya ya Muheza kuwa serikali itamaliza changamoto zinazoukabili mji huo ndani ya muda mfupi, likiwamo tatizo la maji na barabara.

Alisema kuwa kitu ambacho amekuwa akikipigania bungeni ni kuhusu tatizo la maji na kero ya barabara ya kutoka Muheza mjini kwenda tarafa ya Amani kukarabatiwa kwa kiwango cha lami na sasa serikali imemwelewa na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo.

Balozi Adadi alisema kuwa katika mradi wa kutoa maji chanzo cha maji cha Mto Zigi, Tarafa ya Amani kupeleka maji Muheza mjini ambao utagharimu Sh. bilioni 40, utaanza kutekelezwa mwaka kesho.

## Vifo vitokanavyo na uzazi kupunguzwa

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imekusudia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kinamama 556 nchini hadi kufikia 292, mwaka 2020.

Ofisa Programu ya Uzazi Salama kutoka wizara hiyo, Martha Shakinyau, alisema hayo katika uzinduzi wa mradi wa Tulonge Afya pamoja na jukwaa la kusukuma maendeleo ya huduma za afya "Naweza" uliofanyika jijini hapa.

Alisema Wizara ya Afya inakusudia kupunguza zaidi vifo vya uzazi kwa kinamama, wakati wa kujifungua na kabla ya kujifungua kutoka 556 kwa kila 100,000 ya watoto wanaozaliwa wakiwa hai pamoja na vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano hadi kufikia vifo 292 ifikapo 2020, ikiwamo kuokoa watoto wachanga wanaopoteza maisha.

"Takribani kinamama 30 kwa siku hupoteza maisha nchini kutokana na uzazi, hivyo serikali imeona jambo hilo halikubaliki, lazima jitihada za kupambana na janga hilo zihakikishe zinachukuliwa kwa mafanikio makubwa, ili kufikia uchumi wa kati wa viwanda," alisema Shakinyau. Shakinyau alisema kuwa asilimia 63 pekee ya wajawazito ndiyo wanaokwenda kujifungulia katika vituo vya afya ikiwa kwa mwaka wajawazito 2,000,000 hujifungua nchini. Alisema kuwa asilimia 25 ya wajawazito ndiyo wanaoanza kwenda kliniki baada ya kujitambua kuwa ni wajawazito.

Alisema kuwa ifikapo 2020, wizara inatarajia kuwa asilimia70 ya wajawazito watahudhuria kliniki katika vituo vya afya na asilimia 90 waweze kwenda kujifungulia katika vituo hivyo ili kuepuka vifo visivyokuwa vya lazima.

Aidha, alitaja sababu kuu zitokanazo na vifo vya uzazi nchini kwa kinamama hao kuwa asilimia 28 hutokwa na damu nyingi kabla ya wakati wa kujifungua ama baada ya kujifungua, asilimia 17 ni kifafa cha mimba, asilimia 19 kuharibika kwa mimba kwa njia yoyote ile, asilimia 11 ni uchungu pingamizi pamoja na asilimia 14 ni matatizo mengineyo, ikiwamo upungufu wa damu, Ukimwi na malaria.

# Serikali yaagiza waliovamia ardhi kukamatwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imeviagiza vyombo vya ulinzi na usalama vya mkoa na Wilaya ya Kilosa kuwakamata wote wanaotuhumiwa kuwavamia wananchi wanaolima katika mashamba yaliyofutiwa umiliki wake na Rais Dk. John Magufuli mwishoni mwa mwaka juzi.

Agizo hilo la serikali limetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen, alipofanya ziara wilayani humo iliyolenga kujiridhisha utekelezaji wa mashamba yaliyofutwa mwaka 2017 na Rais Dk. Magufuli na kuagiza mashamba hayo kupangiwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kuyagawa kwa wananchi wa maeneo jirani.

Akiwa humo, Dk. Kebwe aliongea na wananchi wa vijiji vya Mvumi na Gongwe ambavyo viko jirani na mashamba hayo matano kati ya 11 yaliyofutiwa umiliki na wananchi waliopewa kuyatumia kwa muda waliwasilisha malalamiko kuwa wamekuwa wakipewa vitisho na baadhi ya watu kwa madai kuwa ni mali yao. Mkuu wa Mkoa wa Morogoro baada ya kupokea malalamiko hayo aliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama kuwakamata wote wanaowatishia wakulima hao.

"Naviagiza vyombo vyote vya ulinzi na usalama, muanze kufanya uchunguzi kuanzia sasa, kama kuna kikundi cha watu au hata mtu binafsi anawatisha wakulima waliopewa mashamba hayo wachukuliwe hatua, kwa sababu sheria zipo," alisema Dk. Kebwe.

Aidha, aliwahakikishia wananchi wa vijiji hivyo kuwa mtu ambaye hana eneo la kulima atapatiwa kupitia mashamba hayo yaliyofutwa ili kila mwananchi aweze kuzalisha na kujikimu kimaisha, huku akionya kutoingiza itikadi ya aina yoyote kwenye mashamba hayo yaliyofutwa. Katika hatua nyingine mkuu huyo, aliwataka wananchi wa vijiji vya Mvumi na Gongwe, kufuata utaratibu uliotolewa na serikali wa kuyatumia mashamba hayo kwa muda wakisubiri mpango rasmi unaoendelea kuandaliwa na serikali, huku akiwaonya wanaotaka kuanzisha mipango mingine ya matumizi ya ardhi hiyo kinyume na mipango ya serikali kusitisha mara moja mipango hiyo.

"Vyombo vyangu vinaniambia wale walikwenda wakavamia maeneo hayo walitaka waanzishe mpango mwingine mpya, yaani juhudi zote hizi ambazo serikali imefanya kwake yeye si kitu, sasa hao mtusaidie tuwafahamu ni kina nani na tuwachukulie hatua, sio kuwafahamu tu," aliongeza Dk. Kebwe. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoyi, amewataka wananchi wa vijiji vya Mvumi na Gongwe kukomesha tabia ya ubishi na ugomvi baina yao, badala yake watekeleze maagizo ya serikali yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa na kuwatahadharisha kuwa atakayekwenda kinyume na maagizo hayo atakamatwa na kuchukuliwa hatua za sheria.

Awali Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda ya Kati, Hezekiely Kitilya, aliewaeleza wananchi wa vijiji vya Mvumi na Gongwe kuwa ardhi ya mashamba hayo matano kwa sasa bado ni ya Rais na iko chini ya Kamishna wa Ardhi na wananchi wamepewa kuitumia kwa muda, hivyo ni vema wakawa watulivu na kuacha ugomvi baina yao.

Kitilya aliwakumbusha wananchi maelekezo yaliyotolewa na Rais baada ya kuyafuta, alisema kipaumbele cha kwanza kinawalenga wananchi wanaozunguka mashamba hayo, cha pili ni kutenga ardhi hiyo kwa ajili ya uwekezaji wenye tija wa ndani na nje ya nchi na kuwa na hazina ya ardhi kwa ajili ya matumizi mengine ya baadaye.

Ofisa Ardhi Wilaya ya Kilosa, Ibrahim Ndembo, alisema mashamba hayo matano Na. 32 hadi 36 yenye jumla ya ekari 2,685, baada ya kufutwa, wilaya ilipeleka maombi serikalini ili kupewa idhini ya kutumia mashamba hayo kwa muda ombi ambalo lilikubaliwa.

Alisema baada ya kukubaliwa na wilaya iliunda kamati za ugawaji maeneo ya mashamba hayo na kuyagawa katika sehemu mbili, ekari 1,000 kwa ajili ya wananchi wa Kijiji cha Mvumi na ekari 1,000 nyingine kwa ajili ya kijiji cha Gongwe.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Dk. Respicious Boniface, akipanda mti wa kumbukumbu katika uzinduzi wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam juzi, ambayo kilele chake ni leo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waagizwa kujenga vituo vya kuteketeza taka za hospitali

**Na George Tarimo**, IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Sima, amewaagiza maofisa mazingira wa wilaya na mikoa kujenga vituo maalumu vya kuteketeza taka ngumu katika hospitali za wilaya na rufani ili kupunguza adha ya kurundikana kwa taka hizo.

Alitoa kauli hiyo katika ziara ya kikazi mkoani Iringa na kusema changamoto kubwa inayozikabili hospitali nyingi nchini ni kukosa maeneo ya kuchomea taka hatarishi hali inayohatarisha afya za wananchi.

Alisema kuwa lengo la ziara hiyo ni kutembelea maeneo ya hospitali pamoja na maeneo yote yaliyozungukwa na Mto Ruaha ili kuendelea kutunza vyanzo vya maji.

Pia kutembelea maeneo ya hafla kuona jinsi takataka hatarishi zinavyoteketezwa kutokana na mengine kutokuwa na vifaa vya kuteketeza taka kama hospitali za rufani na wilaya. Awali akisoma taarifa ya Hospitali ya Wilaya ya Iringa (Frelimo), Mganga Mfawidhi, Philipo Pilila, alisema wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita tano kupeleka taka katika kituo cha Ngome hali ambayo inahatarisha afya za wananchi.

Pililka alisema kuwa changamoto kubwa ndani ya hospitali hiyo ni kukosekana kwa majengo ya kulaza wagonjwa wodi za wanaume, wanawake na watoto na kuwa kukosekana kwake kunasababisha ongezeko la wagonjwa hospitali ya rufani, jengo la kulaza wagonjwa wa magonjwa ya kuambukiza, kukosekana kwa kichomea taka, jengo la utakasaji vifaa, la upasuaji kwa magonjwa mengineyo, chumba cha kuhifadhia maiti, uzio wa hospitali, stoo pamoja na jiko.

Sima alitoa siku 14 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Himidi Njovu, kuteketeza taka zote zilizopo katika eneo la Kihesa Kilolo ambalo ni la maliasili na kutenga eneo maalumu kwa ajili ya wananchi kutupa taka.

"Manispaa hii mmenisikitisha sana kwa sababu ukiangalia hapa mvua imenyesha halafu wananchi wanaenda kutupa taka katikati ya jalala tena maji haya machafu yanashuka kwenda mitaani kitu ambacho ni hatari kwa jamii," alisema Sima. Alisema kuwa ndani ya wiki mbili taka zote ziwe zimeteketezwa na maji yote machafu hayaingii kwa wananchi.

# Wachimbaji wadogo wafundwa kusajili mikataba ya uchimbaji madini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WACHIMBAJI wa madini ya tanzanite Mji mdogo wa Mirerani, wametakiwa kusajili mikataba ya uchimbaji wanaoingia na raia wa nje kwenye Wizara ya Madini.

Ofisa Madini Mkazi wa Simanjiro, Daudi Ntalima, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wachimbaji wa madini ya tanzanite mji mdogo wa Mirerani.

Alisema mikataba yote wanayoingia na wageni inapaswa kusajiliwa wizarani na maelezo yatatolewa ofisini kwao.

Aliongeza kuwa wamiliki wa migodi wanapaswa kupewa utaratibu wa kusajili mikataba hiyo na serikali ikague kubaini namna watakavyonufaika na uwekezaji huo wa wageni.

"Mnapaswa kuishirikisha Wizara ya Madini ili itambue mikataba hiyo na wageni na pia baadaye yasije yakatokea mambo ya kudhulumiana mkashindwa kupata msaada," alisema Ntalima.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justine Nyari, alisema suala hilo watalifikisha kwa wachimbaji wote ili kuhakikisha mikataba yote ya uwekezaji inajulikana na kufikishwa ofisi ya madini.

Alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika uchimbaji madini kwa kuwa wizara ndiyo walezi wa wachimbaji wote nchini hivyo watahakikisha hilo linatekelezwa. "Tukiwa kama wachimbaji madini tutahakikisha utaratibu huo ambao ni mzuri juu ya makubaliano ya wachimbaji na wawekezaji yanatambulika rasmi na serikali kupitia Wizara ya Madini," alisema.

Katibu wa Marema Tawi la Mirerani, Dk. Curtius Msosa, alisema magonjwa ya kifua kikuu na silikosis inayosababishwa na ulanga imewaathiri watu wengi kwenye machimbo hayo. Dk. Msosa alisema watahakikisha wanaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji ili kuhakikisha magonjwa ambayo yanaepukika yanayosababishwa na uchimbaji yanakomeshwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Afya, Usalama na Mazingira migodini wa shirikisho la wachimbaji madini nchini Femata, Dk. Bernard Joseph, alisema watahakikisha masuala ya afya, usalama na mazingira yanapewa kipaumbele.

"Tupo kwenye mchakato wa kuhakikisha vyoo vinajengwa kwa wingi, maji yanapatikana na uchimbaji salama unafanyika migodini kwa manufaa yetu na wachimbaji wetu kwa ujumla migodini," alisema Dk. Joseph.




Mkuu wa Idara ya Masoko na Uhusiano wa Benki ya KCB, Christine Manyeye (kulia), akijibu maswali kutoka kwa wafanyabiashara wa jijini Arusha katika warsha ya Biashara Club, iliyohudhuriwa na wafanyabiashara zaidi ya 250. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya KCB yatoa elimu ya kodi kwa wadau

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BENKI ya KCB Tanzania imetoa elimu ya usimamizi wa fedha, uendeshaji wa biashara na sheria za kodi kwa wafanyabiashara mbalimbali mkoani Arusha.

Wadau mbalimbali katika sekta ya utalii wakiwamo wafanyabiashara walikutanishwa, ambapo sehemu ya kwanza ilikuwa mahususi kwa wateja wa KCB wapatao 250.

Aidha, sehemu ya pili katika mafunzo hayo yalihusu wakazi wengine wa Arusha kupata elimu ya huduma za kibenki kutoka kwa wataalamu wa KCB.

Akizungumza wakati wa kufungua semina hiyo, Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa KCB, Christine Manyenye, alisema wamefanya juhudi mahusus za kuwaleta wadau kama Tanzania National Parks Agency (TANAPA), Mamlaka ya Mapato (TRA), kwa nia ya kujadiliana jinsi ya kutatua baadhi ya changamoto na kupata njia muafaka za kuendeleza sekta ya utalii nchini.

Kwa upande wake Meneja wa Tawi la KCB Arusha, Judith Lubuva, aliwapongeza wafanyabiashara, wadau na wakazi wa Arusha kwa kuhudhuria kongamano hilo na kufafanua kuwa limefanyika wakati muafaka, ambapo sekta ya utalii inaendelea kuimarika katika Kanda ya Kaskazini na Tanzania kwa ujumla.

Mwakilishi TRA, Ombeni Urio, aliyekuwa mshauri wa masuala ya kodi, alisisitiza umuhimu wa wafanyabiashara hao kufuata kanuni za kodi, huku akiipongeza KCB kwa kumwalika ili aweze kutoa elimu hiyo ambayo inahitajika kwa sasa.

# DC Kitundu acharukia wawekezaji wanyanyasaji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, amewaonya wawekezaji wanaowanyanyasa wananchi kwa kuwazuia kuingia katika maeneo yao kupata huduma za kijamii kuacha mara moja.

Alisema wakiendelea kufanya hivyo watakuwa wanaibua migogoro ndani ya jamii.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake juu ya migogoro inayojitokeza wilayani hapa baina ya wawekezaji na wananchi na hatimaye kuzua vurugu zinazokwamisha maendeleo.

"Ni kweli kuna wawekezaji ambao wana maeneo makubwa wanayoyamiliki kihalali na wanalipia kodi serikalini, lakini wamekuwa wakiwazuia wananchi kuingia katika mashamba yao hata kuokota kuni wakati kuna mabaki ya miti iliyokauka na kuoza," alisema Kitundu.

Aidha, alisema wawekezaji wengine wanawazuia wananchi wasiingie kwenye mashamba hayo makubwa wakati hawajayaendeleza, huku wananchi wakiwa wanauhitaji wa huduma ya maji au kuchungia mifugo yao pasipo kuharibu kitu chochote.

Miongoni mwa wawekezaji ambao wanadaiwa kufanya unyanyasaji wa namna hiyo, alidai ni mwekezaji wa asili ya Kiasia ambaye yupo Kijiji cha Malangi anayemiliki eneo kubwa lakini wananchi wakiingia kuchunga mifugo yao au kuchota maji anawafukuza.

Alisema wawekezaji wa namna hiyo wanatakiwa kujiangalia vizuri na kutafuta namna ya kuishi vizuri na wananchi kwa kushirikiana katika ujenzi wa shughuli za maendeleo ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi hata kama wawekezaji wanalipa kodi.

Alitumia fursa hiyo kuvitaka vijiji ambavyo vina wawekezaji na wana maeneo makubwa ambayo hawayaendelezi na vijiji hivyo vina uhitaji wa maeneo ya kujenga miundombinu ya kijamii mfano shule, zahanati na huduma zingine za kijamii kufuata taratibu za kuomba ardhi ili wawekezaji hao wanaomiliki maeneo makubwa waweze kuvipatia maeneo wajenge hiyo miundombinu.

Mkazi wa Babati, Andrew Amos, akizungumza na Nipashe alisema wawekezaji wengi hasa wa kigeni wanaomiliki ardhi kubwa wamekuwa ni mwiba mkali kwa jamii inayowazunguka, huku wakitamba kuwa ardhi hiyo wanaimiliki kisheria.

Mkazi mwingine wa Kiru, Othmani Ramadhan, alisema wawekezaji wakijiwekea mazingira ya kuishi vizuri na jamii watajihakikishia ulinzi wa mashamba yao, lakini watakapowaonea wananchi watachoka na kuanzisha fujo ambayo itawagharimu wawekezaji hao, hivyo ameshauri waishi vizuri na jamii.

# Hospitali ya KCMC kuanza kutumia vipimo vya kisasa mwezi huu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya KCMC inatarajia kuanza kutoa huduma za vipimo vya MRI na CT Scan kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa kuanzia mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo na Katibu wa Shirika la Msamaria Mwema Tanzania, Dk. Gileard Masenga, aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya miaka 48 ya kuanzishwa kwake, miaka 20 ya ushirikiano kati ya KCMC na NORTHUMBRIA NHS ya Uingereza na miaka 10 ya KCRI.

"Mheshimiwa Askofu Dk. Fedrick Shoo, hospitali kwa kushirikiana na wadau wengine imeweza kununua mashine za kisasa za MR na CT Scan kwa gharama ya shilingi za kitanzania bilioni 4.5, ambazo zinasubiriwa kufika na kufungwa kwa ajili ya kusaidia mamia ya wagonjwa wanaotokea katika mikoa mbalimbali ya Tanzania na nchi jirani," alisema.

Mashine za uchunguzi wa magonjwa za MRI (Magnetic Resonance Imaging) na CT Scan (Computerized Tomograph), kazi yake ni kuonyesha mahali penye ugonjwa mwilini na ina wajibu wa kuonyesha ukubwa wa tatizo katika eneo fulani mwilini ambalo hatuwezi kuliona kwa macho.

Kwa mujibu wa Dk. Masenga, mashine hizo zinatarajiwa kuwasili na kuanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi Machi, 2019.

Kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa PACS, mkurugenzi huyo alisema hospitali hiyo pia itaanza kutumia mfumo huo unaohusisha kuondokana na mazoea ya kuhifadhi picha za wagonjwa katika filimu. "Sasa picha hizo zinahifadhiwa kidigitali ambapo daktari anaweza kutazama, kusoma na kutafsiri picha ya mgonjwa popote pale kwenye kompyuta iliyounganishwa na mfumo huu. Mfumo huu umeongeza tija na ufanisi wa idara hii kuwa unapunguza gharama za kudurufu (films) na kurahisisha majibu ya wagonjwa kwa daktari husika," alieleza.

Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, inamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na inasimamiwa na Shirika la Msamaria Mwema (The Good Samaritan Foundation of Tanzania).

Mwaka 2013 ilipandishwa daraja na kuwa "Super Specialist Hospital" yaani hospitali yenye kubobea kwenye fani za upasuaji kwa njia ya tundu dogo (Laparoscopic Surgery), upasuaji kupitia njia ya mkojo pamoja na kibofu cha mkojo (Urology) na matibabu kupitia mfumo wa njia ya chakula, ukitumia mtambo wa darubini ndogo (endoscopic surgery).

Pia imebobea katika upasuaji wa mtoto wa jicho (Cataract Surgery), matibabu ya maradhi ya ngozi pamoja na maradhi ya zinaa (Dermato-venereology).

Kwa sasa, hospitali hiyo ina vitanda 639, lakini idadi ya wagonjwa huwa inaongeka na kusababisha wagonjwa kulala katika korido.

Kwa mujibu wa Dk. Masenga, idadi ya wagonjwa wa nje ni kati ya wagonjwa 600 mpaka 800 kwa sasa na kwamba bado hospitali ina upungufu wa madaktari bingwa na kwa sasa kuna madaktari bingwa 48 tu, ambapo kulitakiwa kuwa na madaktari bingwa 100.

Hospitali ya KCMC imefanikiwa kuboresha huduma katika kitengo cha huduma ya wagonjwa wa nje na wagonjwa wanaolazwa kwa sasa ni zaidi ya 36,470 kwa mwezi na asilimia 79.7 ya wagonjwa wote wanaohudumiwa katika hospitali ya KCMC wanatoka kwenye mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga na Singida.

# Takukuru yawatega wakurugenzi

**Na Paul William,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) 'imewatega' wakurugenzi saba wa halmashauri za wilaya mkoani Kilimanjaro, wanaowatoza ushuru wafanyabiashara wadogo kati ya Sh. 500 hadi 1,000 kwa siku.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Magufuli alisema kwa muda mrefu amekuwa akiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Halmashauri za Wilaya kutoendelea kuwatoza kodi wajasiriamali wadogo maarufu kama machinga ambao mitaji yao haizidi Sh. milioni tatu. Jana,

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kilimanjaro, Holle Makungu, alitoa onyo kwa wakurugenzi hao akiwataka kuacha mara moja kutoza ushuru wajasiriamali hao, zaidi ya hapo atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua. Makungu alisema Rais aliagiza wafanyabiashara waliopatiwa vitambulisho vya ujasiriamali wasibughudhiwe tena.

Alisema pamoja na maelekezo hayo, zipo baadhi ya halmashauri mkoani Kilimanjaro ambazo zinaendelea kuwatoza ushuru wajasiriamali wadogo waliokwishapatiwa vitambulisho vya ujasiriamali ambacho ni kinyume na maagizo ya Rais Magufuli.

Machi mosi mwaka huu, Rais Magufuli alitoa onyo kwa mara nyingine tena kuwa hatamvumilia kiongozi yeyote awe wa mkoa, wilaya au halmashauri ya mji, manispaa au jiji atakayebainika kuhusika kuwatoza ushuru au tozo yoyote kwa wajasiriamali wadogo waliopatiwa vitambulisho.

"Tunazo taarifa za wakurugenzi kuendelea kuwatoza ushuru wajasiriamali wadogo tena wenye vitambulisho vilivyotolewa na Rais Magufuli, huku ni kukiuka maagizo na maelekezo ya Rais wa nchi, Takukuru hatutakubali kuona jambo hili likiendelea," alisema Makungu.

Kutokana na hali hiyo, Makungu ametoa wito kwa wajasiriamali wadogo wenye vitambulisho vya mjasiriamali watakaoendelea kubughudhiwa kwa kudaiwa ushuru wafike ofisi za Takukuru za wilaya iliyo karibu na kutoa taarifa.



Diwani wa Kata Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu (aliyevaa kaptura), akishiriki kubeba mabomba yatakayotumika kuboresha miundombinu ya majitaka katika kata yake juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mahakama yaagiza kuteketezwa dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

JAJI Patricia Fikirini wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, ameamuru kuteketezwa kwa moto dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa kilogramu 10.064 ambazo anadaiwa kukutwa nazo raia wa Liberia, Grace Teta.

Baada ya uamuzi huo wa Jaji Fikiri, mahakama hiyo ilihama kwa muda na kwenda hadi Hospitali ya Rufani ya KCMC kuteketeza dawa hizo katika tanuri kubwa la moto la kuchomea taka.

Akitoa uamuzi huo, Jaji huyo aliagiza bahasha nne zenye dawa hizo za kulevya pamoja na nyaraka za mtuhumiwa huyo zilizokuwa zikishikiliwa Polisi, zikabidhiwe mahakamani hapo.

"Mahakama hii inatoa kibali cha kuteketeza dawa hizo kama alivyoleta ombi hilo Wakili wa Serikali, Agatha Pima. Kwa hiyo bahasha nne zenye dawa hizo zikabidhiwe mahakamani na zitakwenda kuteketezwa leo," alieleza.

Unga huo wa heroin ulikuwa na uzito wa gramu 10,064 sawa na kilogramu 10.064 na zilikuwa zikisafirishwa kuelekea nchini Ghana kupitia Afrika ya Kusini. Novemba 19, mwaka 2013 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (Kia), mwanamke huyo anadaiwa kukamatwa na dawa hizo akitokea nchini Kenya. Raia huyo wa Liberia, alikuwa na hati ya kusafiria, namba 1039080.

Awali kabla ya Jaji huyo kutoa uamuzi huo, Wakili wa Serikali, Agatha Pima, aliieleza mahakama hiyo kwamba shauri hilo lilikuja mahakamani hapo kwa ajili ya kupata kibali cha kwenda kuteketeza dawa hizo.



Ukurasa 14

Kinamama kisiwani Tumbatu walivyyo taabani kulea watoto wanaotelekezwa



Ukurasa 18

Aliyegombea urais Dk. Anna Mghwira afunguka yakwake


# BUFE

Ijumaa Machi 8, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## KYLIE JENNER; BINTI ANAYEKUWA BILIONEA MDOGO ZAIDI DUNIANI

Ukurasa 19



# Wana - Beijing wasimulia walivyorudi na funguo za maendeleo ya kinamama

**Na Yasmine Protace**

SIKU ya Wanawake Duniani, huadhimishwa kila siku kama ya leo, Machi 8 ya mwaka. Ni maadhimisho ambayo nchini yanawawezesha wanawake kukutana na kujadili mambo yao, ikiwamo mikakati na maazimio yanayowahusu.

Ni siku ambayo mara nyingi maadhimisho yake yanapambwa na mabango yenye ujumbe na wengine wakiwa na sare au mavazi yenye ujumbe mahsusi kwa jamii.

Katika siku hiyo, kuna kawaida ya makundi ya wanawake kufanya usafi katika maeneo yanayozunguka jamii na hata kutoa misaada katika vituo vya kulea yatima. Hiyo yote ni sehemu ya kusherehekea.

Tanzania ni kati ya nchi zinazotoa kipaumbele kwa maadhimisho hayo. Historia yake, ilianza kuitwa Siku ya Wafanyakazi Wanawake, ikiadhimishwa kila Machi 8, lengo ni kumuonyesha upendo

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Kinamama kisiwani Tumbat taabani kulea watoto wana

• Inaangukia yatima na wenye wazazi • Tamwa, SOS wajitosa kunusuru h

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

***IKIWA leo ni kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, ambayo mantiki yake ni kutafakari na kukabili nafasi na magumu yanayomkabili mwanamke, bado ukweli upo kuwa kinamama duniani wanakabiliwa na adha kubwa katika nyanja nyingi za maisha. Fuatilia picha ya mkasa wa kisiwani Tumbatu, Unguja na namna unavyokabiliwa.***

WATOTO wanaoishi katika mazingira magumu, wamekuwa wakikosa malezi mazuri na kukosa haki ya zao za msingi, licha ya kwamba Zanzibar imo katika orodha rasmi kimataifa ya wanaolinda haki za watoto.

Mradi wa Malezi Mbadala, inaelezwa kuwa ni mkombozi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa Kisiwa cha Tumbatu, mkoa wa Kaskazini Unguja, ambao umewasaidia kuwatoa katika hali hatarishi, kutokana na ugumu wa maisha kwa familia zao.

Ni mradi ambao unatekelezwa na Kijiji cha Kulea Yatima na Wanaoishi katika Mazingira Magumu (SOS), kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar.

Familia zaidi ya 10 zinazoishi katika mazingira magumu katika kisiwa cha Tumbatu, zimekuwa zikisaidiwa kwa kuwezeshwa kiuchumi, ili kuweza kuwahudumia watoto wao, ikiwamo huduma ya kupata elimu.

Kisiwa cha tumbatu kina zaidi ya wakai 20,000. Shughuli kubwa ya mahali hapo kijijini ni uvuvi na idadi kubwa ya wakazi wake ni wenye kipato cha chini.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mratibu wa Mradi wa Malezi Mbadala kutoka SOS, Nyezuma Simai Iddi, anahimiza umuhimu wa watoto kulelewa katika familia, kuliko vituo vya kulelea yatima au wanaoishi katika mazingira magumu.

Anasisitiza ushirikiano katika malezi na kama mtoto anapopot-



Wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu, wakitembea baada ya kushuka katika usafiri wa jahazi. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN.**

**"Kama tungalikuwa na vizibau vya uokozi pengine asingalipoteza maisha. Ni vyema kwa hivi sasa tuna vizibao hivyo.**



Khadija Omar Kheir, mkazi wa kisiwani Tumbatu akizungumza katika kikao kuhusu malezi mbadala kwa watoto, kisiwani humo.



Miza Mbarouk Je
kwa Mratibu wa
Kaskazini Unguja

BIASHARA

**Wana - Beijing wasimulia walivyorudi na funguo za maendeleo ya kinamama**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Mgombea urais Dk. Anna Mghwira afunguka 'Kinamama na Maendeleo'**

Ukurasa 18


BIASHARA

**Kylie Jenner; Binti anayekuwa bilionea mdogo zaidi duniani**

Ukurasa 19

# tu walivyo otelekezwa

## hali



eza wazazi wake, ushauri mzuri ni vyema familia kushirikiana katika kumkuza katika maadili mema na kumpatia stahiki zake.

"Tusiwe tayari kuwasukuma watoto katika malezi ya vituo, tunashajiisha watoto kulelewa na familia zao tuwe na moyo wa mapenzi na huruma na tuwe na malezi mazuri kwa watoto ili kuijenga jamii yetu" anasema.

Anafafanua kuwa, ni vyema kuwasimamia watoto katika mahitaji yao ya maisha, iwe ya masomo, kuwarekebisha kitabia na kuwasimamia kimaadili.

Nyezuma anasema, serikali imeweka vituo vya kulelea watoto kama njia mbadala. Kwa kawaida mtoto, anapaswa kulelewa na familia inayomzunguka, iwe ndugu au jamaa wa karibu.

"Watoto wanatakiwa kulelewa katika misingi ya upendo kutoka kwa wazazi wa ndugu wa damu. Vituo vya kulelea watoto, ni suluhisho la Mwisho," anasema.

**KIONGOZI TUMBATU**

Sheha wa Shehia ya Tumbatu, Jongowe Miza Ali, Sharif, anasema kwa sasa wanaendelea na kazi ya kutoa elimu kwa jamii, wakiwamo wanaume, kuhusu umuhimu wa kutunza familia na hasa watoto.

Anaeleza kuwa jiografia ya kisiwa cha Tumbatu, kwamba kimezungukwa na bahari hivyo wanaume wa kisiwa hicho shuguhli yao kubwa ni uvuvi na baadhi ya wanaume hao hutelekeza familia zao, hasa pale wanapoenda kufunga kambi nje ya kisiwa, kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

"Katika kisiwa cha Tumbatu, tunalo tatizo la udhalilishaji wa utelekezaji wa familia za mke na watoto unaofanywa na wanaume, ambao huenda Tanzania Bara kwa shughuli za uvuvi na hukaa huko zaidi ya miezi sita, huku wakizisahau kabisa familia zao"anasema.

**WALEZI WAFUNGUKA**

Rahma Ali Khamis (35), ni miongoni mwa walezi waliojitolea na analea watoto watano wa marehemu dada yake, baada ya kutelekezwa na baba yao.

Anasema aliwachukua watoto akiwalea katika mazingira magumu ya maisha, lakini kwa sasa anakiri kupata nafuu, baada ya kusaidiwa na mradi wa malezi mbadala.

Rahma anaeleza kulishukuru shirika la SOS, kwa juhudi zake na kumsaidia watoto watatu, kati ya watano anaowalea, walioingizwa katika mradi huo, akiwa amejengewa nyumba kwa ajili ya kuishi na watoto hao pamoja na kuwezeshwa fedha za miradi ya ujasiriamali.

"Dada yangu amefariki dunia hawa watoto ndio nawalea mimi, lakini baba wa watoto hawa yupo hai, lakini hana huduma yoyote anayoitoa kwa watoto wake," anasema Rahma.

Mlengwa mwingine wa mradi wa malezi mbadala kisiwani humo, Miza Mabrouk Jecha, anaanza kushukuru SOS na Tamwa kwa kubuni wazo la mradi huo, ambao matarajio yake makubwa ni kusaidia kuwawezesha watoto waliokuwa wakiishi katika mazingira magumu.

Mama huyo analea mjukuu mwenye umri wa miezi nane, ambaye mama yake alifariki. Sasa amewezeshwa kiuchumi kupitia mradi huo, ili amudu maisha yake na kumlea mtoto katika mazingira mazuri.

Anaeleza kuwa, kabla ya mradi hali ilikuwa mbaya kiuchumi na alikosa fedha za kujikimu kwa chakula, ili aweze kula na mjukuu mchanga na watoto wake nane.

"Mradi wa malezi mbadala ni mkombozi kwetu, hivi sasa nashukuru namudu angalau milo miwili kwa siku," anasema.

**MKURUGENZI SMZ**

Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Wahida Maabad, anaitaka jamii kubadilika na kurudisha utamaduni wa zamani wa kulea watoto katika mfumo wa familia nzima.

Anasema kwamba, hivi sasa imebainika baadhi ya familia hazipo tayari kulea watoto wa ndugu zao ambao kwa njia moja au nyingine, wamepata matatizo mbali mbali, ikiwamo wazazi wao kufariki.

Wahida anarejea hoja kwamba, nyumba na vituo vya kulea watoto, ni suluhisho la mwisho kwa ajili ya kutunza watoto, pale inapobidi na hatua zingine zimekwama, kwani nafasi kuu ni ya baba, mama na wanandugu wa karibu wa familia.

"Jamii yetu tunaitaka ibadilike na kurudi katika utamaduni wa zamani, kuhakikisha kwamba familia zinatunza watoto na kuacha kuwatelekeza na kuwapeleka katika nyumba za matunzo ya watoto," anasema.



echa, mlengwa wa Mradi wa Malezi Mbadala, akipata maelezo kutoka mradi huo, Nyezuma Simai Iddi, nyumbani Kwake, Tumbatu, Mkoa l.

# UNESCO: Wanawake Afrika uchumi wao umejaa tabu nyingi



Mwanamke akiwa shambani. **PICHA: MTANDAO.**

UKATILI wa kijinsia, uwakilishi mdogo katika uongozi wa tasnia ya habari na kutowezeshwa kujimudu kiuchumi ni moja ya changamoto zinazoendelea kuwakabili wanawake wengi barani Afrika, ikiwamo nchini Tanzania.

Kauli hiyo imetolewa na mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) nchini Tanzania, Tirso Dos Santos, katika ujumbe wake kuelekea siku ya wanawake duniani ambayo kila mwaka hufanyika Machi 8.

Dos Santos, anasema kwa kulitambua hilo, nchini Tanzania, UNESCO imejitoa kupigia upatu wa haki za binadamu, kwa kuwalinda wanawake na kuchagiza mchango wao katika jamii , hasa katika zama zilizopo za utandawazi na digitali wanawake bado wanaachwa nyuma .

Kwa mantiki hiyo anasema: "Ofisi yangu imeweka mipango ya kushughulikia mila potofu zinazowakandamiza wanawake katika jamii, hasa ukatili wa kijinsia ambao ni suala moja linalotia hofu."

Kwa wasichana na vijana, anasema: "Hivi karibuni tumezindua programu ya Afrika nzima, tunaiita programu hiyo 'maisha yetu, haki zetu na mustakabali wetu', na inalenga kuwapa wasichana na vijana elimu kuhusu ngono ili waweze kukabiliana vyema na hali yao katika jamii."

Katika tasnia ya habari, anasema, "Wanawake bado wako nyuma katika ushiriki, tunaona jamii ambayo wanaume ndio waliotawala vyombo vya habari, suala ambalo linahitaji kupatiwa uwiano."

**SULUHU?**

"Ni muhimu kujikita kushughulikia suala la ukatili dhidi ya wanawake wanahabari kwa kuchagiza ushiriki wao katika ngazi zote za mitazamo ya habari, ikiwamo uongozi wa vyombo vya habari", anasema Dos santos. **UN**

UCHUMI

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Wana - Beijing wasimulia walivyorudi na funguo za maendeleo ya kinamama

## • Wataja 'bidhaa' zao; wagombea urais, dawati za jinsia, Tamwa

**INATOKA UK.13**

na heshima, kutokana na mafanikio yake katika nyanja mbalimbali za maisha.

Ni siku ambayo wanawake hutambuliwa kutokana na mafanikio yao, bila ya kujali mgawanyiko wao kitaifa, kabila, lugha, itikadi, utamaduni, kiuchumi au kisiasa.

Siku hiyo inakumbusha jitihada za nyuma na mafanikio na muhimu zaidi kwa ajili ya kuangalia mbele kutokana na uwezo wa wanawake waliopita, kwa manufaa ya kujenga zaidi kizazi kijacho.

### CHIMBUKO LAKE

Chimbuko lake ni Machi 8, mwaka 1857, baada ya wafanyakazi katika kiwanda cha nguo jijini New York, Marekani kugoma, kutokana na mazingira magumu waliokuwa wakikabiliana nayo kiwandani hapo.

Mgomo huo wa uongozi wa kiwanda, ulichukua hatua ya kudhibiti kwa njia ya ukatili na dhuluma. Kinamama hao walifungiwa katika chumba kimoja cha jengo hilo wanawake wote wafanyakazi, bila ya dalili ya huruma dhidi yao na inaelezwa inakadiriwa walikuwa takribani wanawake 129.

Ni tukio lililoibua hisia kali duniani, maelfu ya raia walihudhuria mazishi hayo, jambo linaloifanya tukio kuingia katika vitabu vya historia duniani.


### WALIKUMBUKA DENMARK

Mwaka 1910 nchini Denmark, kulifanyika kongamano la kuwakumbuka wanawake hao na azimio lilipitishwa kuwa Machi 8 ya kila mwaka ifanyike Siku ya Wanawake Duniani, kwa ajili ya kuwakumbuka kinamama hao, ili kuamsha hamasa ya maendeleo kwa wanawake wote.

Pamoja na kwamba siku hiyo ilipingwa vikali na mataifa mengi duniani, kupitia shinikizo la Umoja wa Mataifa (UN), ikaanza kuadhimishwa rasmi mwaka 1975.

Miaka miwili baadaye, Desemba mwaka 1977, Baraza Kuu la UN, lilipitisha na kutangaza kuadhimisha Siku ya Haki za Wanawake na Amani ya Kimataifa. Tangu wakati huo, imekuwa na mwelekeo mpya kimataifa.

UN imekuwa ikisaidia kujenga urithi wa kihistoria hiyo kimataifa kukubali mikakati na viwango vya mipango na malengo ya kuendeleza hali ya maisha kwa wanawake duniani.




Getrude Mongella (aliyesimama), akiongoza mkutano wa Beijing, China. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

> **"Nchini Senegal wanawake walishindwa uvumilivu waliamua 'kubomoa ukuta jijini Beijing, walipoanika yaliyokuwa yanafanyika kwao.**



Mary Rusimbi, Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa TGNP- Mtandao.



Balozi Getrude Mongella; aliongoza Mkutano wa Wanawake Duniani Beijing, China, mwaka 1995.



Profesa Ruth Meena; alishiriki mkutano wa Beijing, China.

Umoja huo na mashirika yake umekuza ushiriki wa kinamama katika kuleta maendeleo endelevu, amani, usalama, na heshima kwa ajili ya haki za binadamu.

Nchini Tanzania, maadhimisho hayo yanafanyika kwa kuwaunganisha wanawake kutoka makundi mbalimbali.

Siku ya Wanawake Duniani, inasisitiza kujenga mshikamano wa wanawake wote duniani, kuhamasisha jamii kutafakari kaulimbiu ya maadhimisho hayo kila mwaka; kuelimisha jamii kuhusu jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali na asasi mbalimbali yakiwamo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Kimsingi, Tanzania kunaelezwa kuwapo mwamko mkubwa wa wanawake kushiriki katika maendeleo na ngazi za uamuzi ikilinganishwa na huko nyuma.

Hiyo inatajwa katika nafasi kama za maamuzi ya kisiasa, kama urais na ubunge na nafasi nyingine za kiutendaji katika umma.

TGNP inaeleza kwamba, kwa kurejea zaidi ya miaka 40 iliyopita, ushiriki wa wanawake bungeni ulikuwa haufiki asilimia 20, wakati hivi sasa imevuka kiwango hicho.

Mwaka 2005, ndipo mwanamke wa kwanza aliandika historia ya kuwania urais. Alikuwa Dk. Anna Senkoro (sasa marehemu), kupitia chama cha PPT- Maendeleo.

Baada ya hapo, wanawake wengine walijitokeza, akiwamo Anna Mghwira wa ACT- Maendeleo mwaka 2015.

Pia, wanatajwa kinamama wengine waliojitosa katika mchakato wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni pamoja; Asha- Rose Migiro na Amina Salum Ali, sasa historia imepiga hatua zaidi kwa nafasi ya Makamu wa Rais kushikwa na mwanamke, Samia Suluhu Hassan.

Pia, nafasi ya Naibu Spika wa Bunge la Tanzania ni mwanamama Dk, Tulia Ackson, akivaa kiatu katika ofisi ambayo alikuwapo, mstaafu Anne Makinda.

### TGNP & BEIJING

Katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, asasi ya TGNP - Mtandao, iliandaa mkutano wa wanawake kutoka maeneo mbalimbali, wakiwamo washiriki mkutano wa Beijing China, ambao Mtanzania, Getrude Mongella, alishiriki kuuongoza, akiwa Mjumbe Maalum wa Umoja wa Mataifa .

Lengo la mkutano huo uliojumuisha nchi zisizopungua 125, lilikuwa ni kutafakari azimio na mpango kazi wa Beijing, huku ikitarajiwa mwaka kesho inatimia miaka 25.

Mwanazuoni wa sayansi ya siasa, Profesa Ruth Meena, anatoa angalizo kwamba, dai la maendeleo endelevu, pasipo kuwapo usawa wa kijinsia hayawezi kufanikiwa.

Profesa Meena, ambaye ni mshiriki wa mkutano huo wa mwaka 1995, anaeleza lengo kuu lilikuwa ni kupata sauti za wanawake ambazo hazifungamani na upande wowote, ikiwa njia mojawapo ya kuleta mabadiliko.

"Tulijifunza mshikamano, ikiwamo na serikali kuwajibika pamoja na mashirika mengine, kwa kuzitambua haki za wanawake," anasema

Profesa Meena, ambaye ni mkongwe aliyetumikia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema kuwa mchakato huo uliwaletea sauti zenye nguvu kwa wanawake, pia madawati ya jinsia yalianzishwa katika taasisi mbalimbali na mashirika mengi.

Mary Rusimbi, ambaye ni mwanzilishi wa TGNP Mtandao na Women Foundation na kushiriki mkutano wa Beijing, anaungana na Profesa Meena kwamba ni mkutano uliozaa matunda wanawake kushika nafasi ya juu ya uongozi, wakiwemo walemavu.

Anasema, ni mikakati yenye maono ya mbali, kugusa kinamama wote wa Afrika Mashariki.

Edda Sanga, ni mwanahabari mkongwe mstaafu, ambaye ana simulizi za kumbukumbu kwamba, badala ya furaha kuna wakati walikumbwa na majonzi yaliyowatoa machozi.

Anasimulia kwamba, nchi za wenzao zilikuwa zinaongelea unyanyasaji na vipigo kwa wanawake, wakati Tanzania walikuwa wakiongelea kufanyishwa kazi, ikiwamo kutembea umbali mrefu.

Anasema baada ya kurudi nchini, wanahabari wakaanzisha Chama cha Waandishi Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), ambayo sasa imebobea katika haki za kinamama na matunda ya juhudi zake yanajulikana.

Edda anasema, nchini Senegal wanawake walishindwa uvumilivu waliamua 'kubomoa ukuta jijini Beijing, walipoanika yaliyokuwa yanafanyika kwao.

"Hiyo ndio ilisaidia kupeleka taarifa Beijing, ili masuala ya wanawake yafanyiwe utetezi," anasema.

Pia, Christina Jesse, anasema wakati wa safari ya Beijing, alikuwa na umri mdogo, anasema, lakini haikuwa kikwazo kushiriki harakati za wanawake wenzake.

Mama huyo ambaye sasa amebobea katika harakati hizo za usawa, anasema alienda katika mkutano huo akitokea katika shirika la kutetea haki za kijamii, anakiri mkutano wa Beijing umeleta matunda makubwa ya kinamama kutambua haki zao.

Anataja mfano wa mafanikio, kama walivyo watangulizi wake, kwamba kuanzishwa madawati ya jinsia katika maeneo mbalimbali ya kusimamia haki za wanawake.

Lingine analolitaja ni kinamama kupewa nafasi za uongozi katika sehemu nyingi, ikiwemo ndani ya fursa za kikatiba.

# Biashara katika picha



Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania Limited, Tarik Moufaddal (kushoto) akizungumza mara baada ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde (wapili kushoto) kukabidhi zawadi kwa washindi wa shindano la Startupper lililoandaliwa na kampuni ya mafuta ya Total Tanzania juzi. Wengine ni mshindi wa kwanza Doreen Noni, mshindi wa pili, Michael Sayi, na mshindi wa tatu, Prince Tillya. **NA MPIGAPICHA WETU**



Utumbo wa ng'ombe ukiuzwa katika mazingira yasiyo salama kwa afya za walaji, katika eneo la Buguruni Kwa Mnyamani, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Mkazi wa jiji, akipita mitaani katika eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana, kukusanya chupa za plastiki kwa ajili ya kwenda kuziuza ili ajipatie riziki. **PICHA: SABATO KASIKA**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 50704.35/-| MAHARAGE 175000.00/-

UCHUMI

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Aliyegombea urais Dk. Anna Mghwira afunguka yakwake



Dk. Anna Mghwira, akipongezwa na Rais, Dk. John Magufuli, baada ya kumuapisha kuwa Mkuu wa Mkoa, Kilimanjaro. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**Na James Lanka,** MOSHI

KATIKA maisha ni vigumu kuweka mpaka kati ya maisha ya kawaida na maendeleo ya kijamii, bila kuhusisha kundi muhimu la wanawake.

Mchango wake unaanzia katika umuhimu wao wa malezi ya watoto, kuanzia wanapozaliwa hadi wanapofikia umri wa kujitegemea, wakitajwa kuwa 'mwalimu wa kwanza' wa binadamu.

Kimsingi, ikitokea wakawalea vibaya watoto tangu wanapozaliwa, basi ni dhahiri kunajengwa taifa lisilo na mwelekeo. Pia, jamii hiyo ya kijinsia inajulikana kuwa na hulka ya kujituma, kujali na kufanya kazi kwa umahiri.

Hata hivyo, inaelezwa kwamba bado watu hao katika jamii nyingi duniani hawajapewa uzito unaostahili kutokana na kuwapo 'mfumo dume' unaoonekana kuwa kikwazo, kwa kudhibiti fursa za kuwapo uwiano sawa katika jamii.

Wakati kesho ni maadhimsho ya Siku ya Wanawake Duniani, kaulimbiu kitaifa ni: "Badili Fikra Kufikia Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu."

**RCMGHWIRA**

Mkoani hapa, Dk. Anna Mghwira, ambaye ni Mkuu wa Mkoa, ana mengi kuhusiana na maendeleo ya Wanawake, akiwa miongoni mwa kinamama wachache waliojitosa kuwania nafasi ya urais, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Akizungumza na Nipashe, kupata utashi wake kuhusu nafasi ya mwanamke, Dk. Mghwira anasema, mila na desturi zilimtenga mbali mwanamke huko nyuma, hali inayomnyima heshima yake.

Dk. Mghwira anasema, Siku ya Wanawake Duniani, inaadhimishwa leo kila wilaya, wakifanya kazi za kijamii zaidi.

Anarejea tukio litakalochukua nafasi wilayani Siha, kwamba wanawake wataenda kushiriki ujenzi wa bweni la wasichana katika moja ya shule za sekondari wilaya humo.

"Katika wilaya ya Same, wataenda kata ya Chome, kwenye ile familia ya mama anayelea watoto watano wenye ulemavu," anafafanua Dk. Mghwira.

> **"Tangu kuanzishwa kwetu mwaka 2009, sisi Shirika la Tusonge tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuyawezesha makundi ya pembezoni, hasa wanawake na vijana katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.**



**WANAWAKE VS VIWANDA**

Akizungumzia katika ushiriki wa wanawake katika kuijenga dunia ya viwanda, Dk Mghwira, anafafanua kuwa wanawake wamekuwa wakihamasisha sana watu kuchangia na katika ujenzi wa dunia ya viwanda.

"Dunia ya Viwanda ilijengwa na wanawake kwenye nchi za Ulaya na Marekani, wakati wa Vita Kuu vya Pili vya Dunia, hasa katika kipindi ambacho wanaume walipokwenda kupigana vitani.

"Wanawake walibaki nyumbani kulea familia, ndipo viwanda vilikuwa kwa haraka, kwa sababu wanawake walitoka majumbani mwao na kuacha familia zao na kwenda kufanya kazi kwenye viwanda hivyo. Nguvu ya mwanamke ni kubwa." anafafanua Dk Mghwira.

Kuhusu nafasui yake, baada ya kuingia katika utumishi sertikalini, Dk Mghwira anafafanua kuwa, bado kuna baadhi ya jamii zimewaweka nyuma wanamke na kusahau mchango wao mkubwa katika uchumi wa nchi.

"Tunampongeza Rais Dk. (John) Magufuli, kwa kutoa nafasi kwa wanawake ambao anaona wanafaa. Mathalani, Makamu wa Rais ni mwanamke na katika mkoa wetu wa Kilimanjaro, mkuu wa mkoa ni mwanamke, katibu tawala ni mwanamke," anasema na kuongeza:

"Ameteua wanawake wengi tu kuwa wakurugenzi, viongozi mbalimbali wa taifa, mikoa na hata katika ngazi za wilaya."

Dk Mghwira anamsifu Rais Dk. Magufuli kwa kuonyesha mfano wa kutoa nafasi mbalimbali kwa wanawake katika kada mbalimbali, zikiwamo za siasa, uchumi na kijamii

**BOSI WA NGO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la Tusonge, linalojishughulisha na Masuala ya uwezeshaji kiuchumi wa wanawake na makundi ya vijana waishio maeneo ya pembezoni, Agnatha Rutazaa, ni vigumu kutenganisha suala la maendeleo katika ngazi zote na uwepo wa mwanamke.

"Tangu kuanzishwa kwetu mwaka 2009, sisi Shirika la Tusonge tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuyawezesha makundi ya pembezoni, hasa wanawake na vijana katika nyanja mbalimbali za kiuchumi," anasema.

Agnatha anaeleza mbinu wanazotumia, ni kutambua vipaumbele vyao na kuvifanyia kazi kwa pamoja, ili kuwaletea maendeleo.

Mwanamama huyo anafafanua kuwa, kupitia mbinu hiyo, wamefanikiwa kupiga vita vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kupitia uanzishaji wa mradi shirikishi wa Vicoba kwa wenye ulemavu na wasio walemavu katika wilaya ya Moshi, mkoa wa Kilimanjaro na jijini Arusha.

Anasema shirika hilo, pia linatoa elimu ya mambo mbalimbali kwa wananchi, ikiwemo suala la Ukimwi na ujasiriamali na imeshaanzisha vikundi vya kuweka na kukopa kwa wajasiriamali wadogo, zikiwemi mahsusi kwa kinamama

Mama huyo anataja siri ya mafanikio ni ushawishi walioujenga kwa umma kupitia mbinu mbalimbali.

FEDHA >> USD 2300.38| Pauni 3065.26| Euro 2619.21

UCHUMI

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Kylie Jenner; Binti anayekuwa bilionea mdogo zaidi duniani

• Umri miaka 21, fedha Sh. trilioni 828

Na Mwandishi Wetu



Kylie Jenner, akiwa na mwanawe. **PICHA: MTANDAO**

MAAJABU na kweli. Sasa 'wanawake wanaweza. Binti wa Kimarekani, Kylie Jenner, akiwa na miaka 21 tu, ameingia katika rekodi ya mabilionea duniani, kwa mujibu wa orodha ya mabilionea iliyotolewa na gazeti la Forbes, linalochapishwa nchini Marekani.

Jenner, ambaye ndiye mdogo zaidi katika familia ya Kardashian, amepata utajiri wake kutokana na biashara ya vipodozi.

Akiwa na umri wa miaka 21, alianzisha na kumiliki kampuni ya vipodozi iitwayo Kylie Cosmetics, biashara ya urembo ambayo imedumu miaka mitatu sasa na kumuingizia mapato ya takriban Dola za Marekani milioni 360 (Sh. Trilioni 828) mwaka jana.

Alifikia mafanikio haya mapema kuliko muasisi wa mtandao wa kijamii wa Facebook, Mark Zuckerberg aliyekuwa bilionea akiwa na umri wa miaka 23.

"Sikutarajia chochote. Sikujua hali ya baadae. Lakini, kutambuliwa inafurahisha. Ni jambo zuri la kunitia moyo," Jenner aliliambia jarida la Forbes.

Orodha ya Forbes inaonyesha muasisi wa The List Shows Amazon, Jeff Bezos, akiendelea kushikilia nafasi ya kwanza kwa binadamu tajiri zaidi duniani.

Jumla ya utajiri wake ni Dola za Marekani bilioni 131 ikiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 19 kutoka mwaka 2018.

Lakini, kiwango cha mapato ya mabilionea wote kwa ujumla kimeshuka kutoka Dola za Marekani trilioni 9.1.

Miongoni mwa mabilionea ambao utajiri wao unapungua ni mwanzilishi wa Facebook Mark Zuckerberg.

Umeshuka kwa Dola za Marekani, bilioni 8.7 katika kipindi cha mwaka uliopita kwa dola za Marekani bilioni 62, kwa mujibu wa orodha ya jarida la Forbes

Hisa zake katika Facebook, wakati mmoja zilipungua kwa thamani yake ya theluthi moja wakati kampuni ilipokuwa ikikabiliana na kashfa.

Hisa za kampuni ya mauzo ya mtandaoni ya Amazon, zimefanya vizuri na hivyo kuboresha akaunti za benki za Bezos na mwanya kati yake na Bill Gates, ambaye yupo katika nafasi ya pili ni mpana kiasi, ingawa utajiri wa Gates, umepanda kwa dola za Marekani bilioni 96.5 kutoka Dola za Marekani bilioni 90 alizokuwa nazo mwaka jana.

Kwa mabilionea wote waliotajwa kwenye orodha hiyo, ni

> **Sikutarajia chochote. Sikujua hali ya baadae. Lakini, kutambuliwa inafurahisha. Ni jambo zuri la kunitia moyo.**

wanawake 252 tu na mwanamke tajiri zaidi aliyejitafutia utajiri mwenyewe ni mogul Wu Yajun wa ChIna, kupitia kampuni yake ya makazi , akiwa na utajiri wenye thamani ya takriban Dola bilioni za Marekani bilioni 9.4.

Idadi ya wanawake waliojitafutia utajiri wao imeongezeka kwa mara ya kwanza na kufikia hadi wanawake 72 kutoka wanawake 56 mwaka jana.

Orodha ya jarida la The Forbes ya mabilionea, ni kielelezo cha utajiri cha tarehe 8 Februari 2019.

Gazeti hilo hutumia viwango vya bei katika masoko ya hisa vya siku hiyo na viwango wa mauzo ya pesa kutoka kote duniani.

Kulingana na Forbes kuna mabilionea wachache wakiwamo takribani 2,153 miongoni mwao wakiwa katika orodha ya mwaka 2019, kiwango hicho kikiwa kimeshuka ambapo mwaka 2018 walikuwa 2,208. Kwa sehemu moja, hii inaelezea ni kwa nini wastani wa utajiri wao ni sawa na thamani ya dola za Marekani bilioni 4, ikiwa ni chini ya Dola za Marekani bilioni 4.1.

Forbes pia ilibaini kwamba mabilionea 994, hali zao za utajiri sasa si nzuri ikilinganishwa na mwaka jana.

Luisa Kroll, ambaye ni Naibu Mhariri wa masuala ya utajiri katika jarida la Forbes, anasema:"Hata nyakati za mtikisiko wa uchumu na rasilimali mjasiliamali hupata njia za kupata utajiri."

Kuna raia 52 wa Uingereza kwenye orodha. Walioko juu ni Hinduja brothers, Srichand na Gopichand, ambao wanamiliki Hinduja Group, wakiwa na jumla ya utajiri wenye thamani ya dola za Marekani bilioni 16.9.

Nyuma yao ni James Ratcliffe, muasisi wa kampuni ya kemikali ya Ineos, mwenye utajiri wa dola bilioni za Marekani 12.1, ambaye ametajwa kama tajiri binafsi.

Tajiri mwingine anayeibuka ni Safra Catz, ambaye ni Mkurugenzi mwenza wa kampuni ya programu ya Oracle, ambaye kwa mujibu wa jarida, huingiza mapato ya Dola za Marekani milioni 41 ya mshahara.

Marekani kunaelezwa kuwapo mabilionea 607, idadi hiyo ikiwa ni kubwa kuliko nchi nyingine yoyote duniani.

China inachukua nafasi ya pili ikiwa na mabilionea 324. Lakini, orodha ya mabilionea imeshuhudia mabadiliko makubwa; - ina mabilionea wapya 44 kwenye orodha huku 102 wakitoka kwenye orodha hiyo.

Kushuka kwa thamani ya pesa ya Euro, kunaelezwa kumewaponza mabilionea wa Ulaya ambao hawakujitokeza kwa wingi kwenye orodha ya matajiri wa dunia, huku wakionekana wawili tu miongoni mwa watu 20 tajiri zaidi dunia.

Mkurugenzi mkuu wa kampuni ya Ufaransa ya bidhaa za burudani LVMH, Bernard Arnault (aliwekwa nafasi ya nne) na muasisi wa kampuni ya Index inayomiliki maduka kama Zara-Amancio Ortega (akaorodheshwa katika nafasi ya 6 ).

Forbes linasema kuwa watu 247waliokuwemo kwenye orodha ya mabilionea mwaka jana kwa sasa wametoka. Miongoni mwao ni Domenico Dolce na Stefano Gabbana, wanamitindo na waanzilishi wa Dolce & Gabbana.

Mwenyekiti wa kampuni ya usambazaji wa bidhaa Li & Fung, Victor Fung, pia hayupo tena katika orodha ya mabilionea wa jarida la Forbes, baada ya kuwapo kwenye orodha hiyo kwa miaka 18. BBC

***• Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Machi 3, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Manyara | Mbeya | Morogoro | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 43,000 | 70,000 | 47,000 | 60,000 | 48,000 | 54,000 | 54,000 | 40,000 | 49,000 | 62,000 |
| Mchele | 200,000 | 230,000 | 190,000 | 185,000 | 180,000 | 180,000 | 200,000 | 185,000 | 170,000 | 180,000 |
| Mtama | 35,000 | 60,000 | 35,000 | 100,000 | 80,000 | 80,000 | 42,000 | 105,000 | 100,000 | NA |
| Uwele | 40,000 | 70,000 | 36,000 | 110,000 | NA | 60,000 | 100,000 | NA | 100,000 | 150,000 |
| Ulezi | 73,000 | 140,000 | 85,000 | 150,000 | 180,000 | 150,000 | 120,000 | 115,000 | 180,000 | 160,000 |
| Ngano | 80,000 | 130,000 | 160,000 | NA | 100,000 | 150,000 | 120,000 | 120,000 | 150,000 | NA |
| Maharage | 160,000 | 220,000 | 165,000 | 150,000 | 180,000 | 130,000 | 150,000 | 180,000 | 180,000 | 170,000 |
| Viazi Mviringo | 65,000 | 75,000 | 65,000 | 75,000 | 65,000 | 90,000 | 50,000 | 50,000 | 80,000 | 70,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Machi 6, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,491.31 | -49.33 |
| DSEI | 2,087.94 | +7.31 |
| Thamani za Hisa (bln) | 20,125.46 | |
| Mauzo | 1,098,241,300.00 | |
| Hisa | 234,477 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| SWIS | 2,000 | -14.53% |
| USL | 10 | -33.33% |
| NICO | 160 | +6.67% |
| KCB | 990 | +2.06% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

### Bei za hisa hadi kikao cha Machi 6, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TCCL | 600 | 600 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TBL | 11,400 | 11,800 | -3.39 |
| SWIS | 2,000 | 2,340 | -14.53 |
| SWALA | 490 | 490 | +0.00 |
| PAL | 400 | 400 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |
| NICO | 160 | 150 | +6.67 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MBP | 490 | 490 | +0.00 |
| KCB | 990 | 970 | +2.06 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| CRDB | 135 | 135 | +0.00 |
| ACA | 6,200 | 6,200 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,020 | 2,020 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |
| USL | 10 | 15 | -33.33 |
| VODA | 800 | 800 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.80 | 22.98 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.62 |
| RWANDAN FRANC | 2.53 | 2.56 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.20 |
| USD | 2277.50 | 2300.27 |
| POUND STG | 2992.40 | 3022.55 |
| EURO | 2573.80 | 2600.69 |
| CANADIAN $ | 1701.15 | 1717.52 |
| SWITZ. FRANC | 2266.84 | 2289.28 |
| JAPANESE YEN | 20.37 | 20.57 |
| SWEDISH KRONOR | 244.29 | 246.63 |
| NORWEG. KRONOR | 262.49 | 265.00 |
| DANISH KRONOR | 345.08 | 348.48 |
| AUSTRALIAN $ | 1601.31 | 1617.78 |
| INDIAN RPS | 32.43 | 32.73 |
| PAKISTAN RPS | 15.61 | 16.31 |
| ZAMBIAN KWACHA | 187.89 | 190.89 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.11 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.21 | 36.51 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3170.57 | 3202.27 |
| GOLD (T/O) | 2930131.75 | 2960171.46 |
| S. AFRICAN RAND | 160.25 | 161.77 |
| UAE DIRHAM | 620.13 | 626.16 |
| SINGAPORE $ | 1677.59 | 1694.12 |
| HONK KONG $ | 290.13 | 293.03 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 607.30 | 613.34 |
| KUWAIT DINAR | 7491.76 | 7560.96 |
| BOTSWANA PULA | 212.95 | 216.92 |
| CHINESE YUAN | 339.55 | 342.83 |
| MALAYSIA RINGGIT | 557.25 | 562.28 |
| SOUTH KOREA WON | 2.02 | 2.04 |
| NEWZEALAND | 1543.23 | 1559.35 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **6/Mar/2019** | **4.10** | **2,310.00** | **2,298.96** | **2,300.27** |
| 5/Mar/2019 | 3.70 | 2,313.00 | 2,398.90 | 2,300.29 |
| 4/Mar/2019 | 4.65 | 2,313.80 | 2,298.85 | 2,300.32 |
| 1/Mar/2019 | 4.60 | 2,314.00 | 2,298.80 | 2,300.36 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **6/Mar/2019** | **71,700** | **6.50** | **4.00** | **5.42** |
| 5/Mar/2019 | 61,000 | 5.00 | 4.00 | 4.89 |
| 4/Mar/2019 | 57,900 | 6.50 | 4.75 | 4.90 |
| 1/Mar/2019 | 60,000 | 5.00 | 4.75 | 4.85 |
| 28/Feb/2019 | 28,000 | 4.75 | 4.67 | 4.74 |
| 27/Feb/2019 | 39,000 | 4.75 | 4.75 | 4.75 |

# Afrika inaelekea pazuri kujikomboa kiuchumi

**Yaoundé,** Cameroon

WATAALAMU wa Umoja wa Afrika, wanasema bara hilo linaelekea pazuri katika kujikomboa kiuchumi, kutokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na mataifa mbalimbali, kurekebisha mikakati yao kiuchumi.

Ni kauli katika mkutano wa kiufundi wa mawaziri wa fedha, uchumi, mipango na ushirikiano wa kikanda unaoendelea mjini Yaoundé, Cameroon.

Akizungumza na idhaa ya Kiswahili ya Radio Ufaransa, mtaalamu wa Sera za Uchumi na Utafiti kutoka Umoja wa Afrika, Dk. Ligane Msene, anasema nchi za Afrika zimeonyesha kupiga hatua kubwa katika mchakato wa uanzishaji viwanda, hali inayochangia kuongezeka uzalishaji wa bidhaa Afrika.

"Ukiangalia, sio rahisi kuona hatua zilizopigwa, lakini Afrika imepiga hatua katika mchakato wa viwanda, sababu kwa leo idadi ya vitu vilivyotengenezwa barani Afrika imeongezeka," anasema.

Dk. Sene anasema, maendeleo hayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukua kwa teknolojia, ambayo nchi wanachama zimeanza kuona umuhimu wake katika kujikwamua kiuchumi na kuongeza kasi ya uzalishaji.

Anafafanua kwamba, kupanuka teknolojia ya mawasiliano, pia kumechangia kiasi kikubwa kurahisisha mwingiliano kati ya nchi moja na nyingine.

Mara nyingi ni jambo linalosaidia sana kuchochea azma ya Umoja wa Afrika ya kuwa na ushirikiano imara wa kikanda na kufanya biashara baina ya nchi wanachama.

"Maendeleo hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa kidigitali barani Afrika. Pia, kutokana na ongezeko la washirika wa kibiashara. Sasa Afrika inafanya biashara na Wachina, Wahindi, jambo litakaloimarisha teknolojia kiasi kwamba, bidhaa kutoka barani Afrika, zitakuwa na uwezo wa kushindana na bidhaa za mataifa mengine katika soko".

Kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya uzalishaji, ni suala ambalo Dk. Sene analisisitiza kwamba linaongeza kasi ya kukabiliana na changamoto... 

Anaitaja kwamba, ni hatua ya kwanza katika kutengeneza fursa ya kupanua masoko kwa kampuni nyingi zaidi barani Afrika, ili kusambaza bidhaa zao nje.

Kuhusu janga la wahamiaji, hasa vijana wanaotoka barani Afrika kwenda Ulaya kutafuta maisha, Dk. Sene anasema ni lazima bara litofautishe sababu zinazowafanya vijana kuamua kupanda meli kwenda Ulaya, kupitia njia ambazo si salama na zinazohatarisha maisha yao.

Dk. Sene, pia anataja sababu kubwa ya vijana kukimbia nchi zao, ni hali ngumu ya uchumi majumbani na ukosefu wa ajira, mambo anayoyaeleza yanaweza kutatuliwa. Anataja mbinu za utatuzi ni za Kiafrika kutengeneza mazingira bora ya ajira na kuboresha hali ya maisha ya raia wake, ili wabaki katika nchi zao.

"Kwangu mimi, nafikiri inabidi kukabiliana na sababu maalum ya watu kuhama ambapo sababu kubwa ni maendeleo hasi na ukosefu wa ajira kwa vijana hao", anasisitiza.

Mtaalamu huyo anaongeza kuwa bara la Afrika lina rasilimali nyingi kama vile gesi, mafuta na madini, anazozitaja ikiwa zitatumika kwa uaminifu, zinaweza kubadilisha kabisa taswira ya bara la Afrika kiuchumi.

Anasema, imefika wakati wa viongozi wa Afrika waamue na kutambua utajiri mkubwa ambao bara hilo linao, kwa ajili ya kubadili maisha ya raia wake.

Katika mkutano huo, karibu wajumbe wote wamekubaliana kuharakisha mchakato wa upitishaji miradi ya maendeleo kwa Bara la Afrika, huku wakisisitiza suala la utawala na mapambano dhidi ya rushwa, mambo anayoyasema yanaikwamisha Afrika. Radio Ufaransa **(RFI).**




Viongozi wa Afrika katika moja ya vikao vinavyowahusu. **PICHA: MTANDAO.**



## HABARI MBEYA

# Wazazi waweka mikakati mipya kukabiliana ubakaji wa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZAZI na walezi wa kitongoji cha Mageuzi, Kata ya Nsalala katika Wilaya ya Mbeya, wameanza kutekeleza agizo la Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo la kuwapeleka shuleni na kuwarudisha nyumbani wanafunzi wa shule za msingi ili kulinda usalama wao kutokana na kuibuka kwa vitendo vya ubakaji.

Wakizungumza na Nipashe jana wazazi hao walisema kuwa wamelazimika kufanya hivyo kutokana na kushamiri kwa matukio ya ubakaji kwa watoto walio na umri wa mitatu mpaka 12.

Mmoja wa wananchi hao, Anna Lucas, alisema wameamua kutekeleza agizo hilo na kwamba wanalazimika kufanya hivyo kwa lengo la kulinda usalama wa watoto wao hususan wanapokwenda shule na kurejea majumbani.

Alisema maagizo ya wazazi kuongeza usimamizi na ulinzi kwa watoto ikiwa ni pamoja na kuwapeleka shule na kuwarudisha nyumbani ulitolewa kwenye mkutano wa kitongoji baada ya kuripotiwa matukio kadhaa ya watoto kubakwa.

"Matukio ya ubakaji ndiyo yametuamsha wazazi na kujua majukumu yetu ya kuhakikisha watoto wetu wanaendelea kuwa salama, maagizo ya ofisa mtendaji yanataka kila mzazi kabla ya kwenda kwenye majukumu yake ampeleke mtoto shule," alisema Anna.

Akizungumzia utekelezaji wa wazazi kuwalinda watoto, Diwani wa Kata ya Nsalala, Kisman Mwangomale, anaamini kupitia utekelezaji huo vitendo vya ubakaji vitapungua.

Pia alisisitiza wanafunzi wote wa shule za msingi kutembea kwa makundi na kutumia barabara kuu zinazounganisha mtaa na mtaa ili kulinda usalama wao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Nsalala, Christina Mwaisela, alisema kwa sasa matukio ya ubakaji hayajaripotiwa kutokana na ushirikiano uliopo baina ya wazazi, viongozi wa serikali za mitaa na walimu.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima (katikati), akizungumza baada ya kutembelea dampo la Kihesa Kilolo lilipo katika Kata ya Kihesa Manispaa ya Iringa. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela na Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) Mkoa wa Iringa, Ritha Kabati. **PICHA: OMR**

# Uhaba vitendea kazi wakwamisha Zimamoto kujitanua

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limeshindwa kufungua vituo vya kutolea huduma zake kwa wananchi katika baadhi ya wilaya za Mkoa wa Mbeya kutokana na uhaba wa vitendea kazi ikiwamo uchache wa magari ya kuzima moto.

Hayo yalisemwa jana na Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Baraza Mvano, wakati akipokea gari la kuzima moto ambalo limetolewa na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson.

Akipokea gari hilo, Mvano alisema kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mbeya linakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi pamoja na uchache wa askari, jambo ambalo linakwamisha kupanua shughuli zake wilayani.

"Tunakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa vitendea kazi, hasa magari ya kuzimia moto hali ambayo inasababisha tushindwe kufungua ofisi za kutolea huduma zetu katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya," alisema Mvano.

Alisema kwa sasa ofisi za kutolea huduma ya Jeshi la Zimamoto na Ukoaji zimefunguliwa katika wilaya za Mbeya, Rungwe na Mbarali pekee, huku wilaya za Chunya, Kyela pamoja na Halmashauri ya Busokelo zikikosa huduma hizo.

Naibu Spika Dk.Tulia jana alikabidhi magari mawili kwa uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kati yake moja likiwa ni la kuzima moto na lingine likiwa ni la maji taka.

Akikabidhi magari hayo, Dk. Tulia alisema kuwa lengo ni kuboresha huduma kwa wananchi ili kuwaletea maendeleo ikiwa ni sehemu ya jitihada zake za kuunga mkono serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Nimeamua kuleta magari haya ambayo thamani yake ni zaidi ya shilingi milioni 600 ili yatumike kuboresha huduma kwa wananchi. Jiji la Mbeya limekuwa likipata matukio mengi ya moto kuteketeza mali za wananchi, hivyo nimeona ni vizuri kuleta gari hili kwa ajili ya kutolea huduma za kuzima moto," alisema Dk. Tulia.

"Pia na tambua kuwa Jiji la Mbeya lina changamoto ya huduma ya uondoaji wa maji taka hasa kwa kuzingatia kuwa gari lililopo haliko kwenye hali nzuri, hivyo katika eneo hilo pia nimeleta gari la kuzolea maji taka kwa lengo la kuboresha huduma za uondoaji wa maji taka ili kulinda afya za wakazi wa Jiji la Mbeya," aliongeza Dk. Tulia.

Dk. Tulia alisema ataendelea kushirikiana na wananchi katika kutatua changamoto zinazowakabili katika nyanja mbalimbali ili kuwafanya wananchi wajikite kwenye shughuli za kuwaletea maendeleo badala ya kuhangaika kukabiliana na changamoto nyingine ambazo ni kikwazo katika shughuli zao za kimaendeleo.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, alimshukuru Dk. Tulia kwa msaada huo akidai kuwa kwa kufanya hivyo anachangia katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015.

# Matundu 48 ya vyoo kutafuna mil. 25/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIASI cha Sh. milioni 25 kinahitajika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa matundu 48 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Malama iliyopo Kata ya Nsalala wilayani Mbeya.

Diwani wa Kata ya Nsalala, Kisman Mwangomale, alisema shule hiyo kwa sasa ina matundu ya vyoo 24, ambayo kati yake matundu 12 yanatumiwa na wanafunzi wa kike na mengine 12 ni kwa ajili ya watoto wa kiume.

Alisema matundu hayo ya vyoo hayakidhi mahitaji ya shule hiyo ambayo ina wanafunzi 600 na hivyo kusababisha kuwapo kwa haja ya kujenga choo chenye matundu mengine 48 ili kupunguza changamoto hiyo.


Diwani Mwangomale alisema kuwa katika kukabiliana na changamoto hiyo, wananchi kwa kutumia nguvu zao wameanzisha mradi wa ujenzi wa vyoo vipya shuleni hapo, mradi ambao alidai kuwa unahitaji zaidi ya shilingi milioni 25 kuukamilisha.

Aliwataka wananchi wa Kata ya Nsalala pamoja na wadau wengine ikiwamo serikali kujitokeza kusaidia kukamilisha mradi huo wa vyoo ili kuepusha wanafunzi hao kupatwa na magonjwa ya mlipuko.

"Ninaomba wadau wengine ikiwamo serikali wajitokeze kushirikiana na wananchi wangu kuendeleza na kukamilisha mradi huu kwa lengo la kunusuru watoto wanaosoma katika shule hii na magonjwa ya milipuko yanayoweza kuwapata, lakini pia kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kujisomea," alisema Diwani Mwangomale.

Aidha, alisema kuwa mwitikio mkubwa wa wazazi wa kuwapeleka watoto shule nayo imekuwa ni changamoto kubwa kwenye kata hiyo hususan katika shule za msingi ambako pia imeibuka changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa na miundombinu mingine.

Mkazi wa Nsalala Sarafina John, alisema wananchi kwa kushirikiana na serikali wapo tayari kuchangia ujenzi wa vyoo ili wanafunzi waendelee kusoma bila bugudha.





# Dk. Mahenge atoa agizo zito ujenzi wa Jiji la Dodoma

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameitaka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhakikisha inadhibiti ujenzi holela ili liwe jiji lenye mpangilio mzuri.

Dk. Mahenge alitoa kauli hiyo jana, baada ya kukagua miradi ya upimaji wa viwanja katika kata ya Mtumba na Mapinduzi jijini humo.

Alisema kupimwa kwa maeneo hayo kuna toa fursa kwa wananchi kumiliki viwanja vilivyopimwa kulingana na mahitaji yao, hivyo hakuna sababu ya kujenga kiholela.

"Acheni kununua maeneo yasiyopimwa ili kuepusha migogoro ya ardhi na ununuaji huu unasababisha mnajenga holela, nataka Jiji la Dodoma mdhibiti ujenzi holela ili liwe jiji la mfano la kuigwa na majiji mengine makubwa," alisema.

Aidha, aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa ya upatikanaji wa viwanja katika jiji hilo ili waweze kuwekeza Dodoma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, aliwaomba wawekezaji kutumia fursa hiyo kuwekeza Dodoma kwa kuwa vipo viwanja vya kutosha.

Alisema kuwa halmashauri hiyo inaendelea na mkakati wa kuboresha makazi ambayo hayakuwa rasmi na kupima maeneo mapya.

"Tunaalika kampuni zote kuwa Dodoma ni sehemu salama kwa ajili ya uwekezaji, viwanja vipo, miundombinu iko lakini pia kampuni za upimaji ardhi tunazikaribisha," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema sehemu kubwa ilikuwa ni malalamiko ya ulipaji wa fidia kwa wananchi kwenye maeneo yaliyotwaliwa na serikali au yaliyovamiwa na suala hilo limeshughulikiwa.

"Watu wameshalipwa fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa na serikali, lakini wengine wamepewa maeneo mbadala pamoja na kwamba walivamia maeneo hayo," alisema.



Makamu Rais wa kampuni ya Korea ya Radian Qbio ambayo imegundua kifaa cha kupima magonjwa mbalimbali ikiwamo virusi vya Ukimwi, ebola na magonjwa mengine, Kim Taehwan (kulia), akisisitiza jambo kwa Katibu wa Bunge, Stephen Kigaigai (kushoto), wakati yeye na ujumbe wake walipomtembelea ofisini kwake, mjini Dodoma jana, kabla ya kutambulisha kifaa hicho. Katikati ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Kim Beom Ki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa ataka mamlaka za maji kufika vijijini

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

WAZIRI wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, amezitaka mamlaka za maji nchini kuacha kujikita kwenye maeneo ya mijini pekee bali wafike na vijijini kwa kuwa ndio kwenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji.

Aidha, amesema kuwa kuanzishwa kwa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) kutasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mbarawa aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akifungua kikao kazi cha wadau wa maji kuhusu sheria mpya ya maji na usafi wa mazingira ya mwaka 2019, pamoja na uanzishwaji wa wakala wa usambazaji maji vijijini (Ruwasa).

Alisema sheria mpya ya maji namba 5 ya mwaka 2019 tayari imeshasainiwa na Rais, hivyo kikao hicho cha wadau wa maji kitatumika katika kuhakikisha kuwa wanajadili na kutoa mapendekezo yao mbalimbali ili kuweza kuboresha.

"Unakuta mamlaka kiwango cha upatikalnaji wa maji katika eneo la mjini lipo juu sana, lakini ukitembea kijijini kidogo unakuta shida kubwa ya upatikanaji wa maji, wananchi wanahangaika kutafuta huduma hiyo," alisema.

Alifafanua hivi sasa hali ya upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 56.8, hivyo jitihada zinahitajika ili kuweza kufikia asilimia 85 ifikapo 2020 kama ambavyo ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 inavyoelekeza.

"Kuanzishwa kwa wakala wa usambazaji maji mijini na vijijini kutasaidia sana kutufikisha katika kufikia asilimia 85 ya upatikanaji maji vijijini, kwa kuwa hata jukumu la uchimbaji visima na mabwawa litakabidhiwa kwa Ruwasa," alisema.

Aidha, alisema kuwa kuundwa kwa sheria ya maji na usafi wa mazingira kutasaidia kujibu changamoto zilizopo katika huduma za maji katika maeneo mengi nchini.

Naye Mkuregenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (Dawasco), Cyprian Luhemeja, alisema kuwa moja ya changamoto katika mamlaka nyingi nchini ni upotevu wa maji.

Alisema hivi sasa Dawasco wamejipanga kuhakikisha kiwango cha upotevu wa maji kinapungua hadi kufikia asilimia 25 kutoka 49 aliyoikuta toka alipoteuliwa kuwa mkurugenzi wa mamlaka hiyo.

# Jamii yaombwa kujitoa kwa kusaidia yatima

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JAMII imeombwa kujitokeza kusaidia watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu katika maeneo mbalimbali nchini ili waweze kupata haki za msingi ikiwamo elimu.

Wito huo ulitolewa jana na mlezi wa kituo cha kulea watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu cha Rahmani kilichopo Chang'ombe Juu jijini hapo, Rukia Hamisi, alipokuwa akizungumza na Nipashe kituoni hapo.

Hamisi alisema kumekuwa na ongezeko la watoto hao, hivyo ni wajibu wa jamii kusaidia watoto hao kuwatunza ili waweze kupata mahitaji ya msingi kama watoto wengine.

"Kwa mfano hivi majuzi Ofisi ya Ustawi wametuletea watoto wawili wa chini ya miaka mitano hawajulikani hata majina yao, walitelekezwa na mzazi wao njiani, idadi ya watoto inaongezeka kila siku na mahitaji hivyo wasamaria wema wanahitajika," alisema.

Alisema kuwa kituo hicho kinatunza watoto yatima zaidi ya 100 na kati ya hao wanaoishi kituoni ni watoto 50 na idadi iliyobaki ni wale wanaoishi majumbani kwao kwa kusaidiwa mahitaji na kituo.

Alibainisha kuwa watoto hao wanatoka katika mikoa mbalimbali na wengine hawajulikani wazazi wao kutokana na kupelekwa hapo na ustawi wa jamii.

Aidha, alisema kituo hakina wafadhili kinategemea wasamaria wema kujitokeza kuwasaidia mahitaji mbalimbali kwa ajili ya watoto hao.

Hamisi alisema wakati wa mwezi Ramadhani kuna wasamari wema wengi hujitokeza kuwapelekea misaada ambayo huwasaidia kwa kiasi kikubwa.


"Pia tunamshukuru Mungu kumekuwa na watu wakifika na kutoa misaada ya vitu mbalimbali, lakini haitoshelezi ila tunawaomba na wengine wajitokeze kusaidia," alisema.

Hata hivyo alisema kuna kinamama wa maeneo hayo wamekuwa wakiwasaidia vitu vidogo vidogo pamoja na kuwafulia watoto nguo zao na usafi wa kituo kila baada ya siku chache.

Aliyataja mahitaji makubwa wanayohitaji watoto hao kuwa ni chakula, mavazi kwa jinsia zote mbili na mahitaji ya daftari na sare za shule kwa wale wanaosoma.

Kadhalika, alisema wamejipanga kutanua kituo hicho ili kiweze kuanzisha mradi wa ushonaji ambao utasaidia kupata fedha za kuhudumia watoto.

"Tunaomba wadau wakumbuke na hiki kituo kuna watoto wanahitaji msaada wao," alisema.







Frateri Baraka Denis Mchechu (kushoto), akiwapaka majivu waumini kwenye Ibada ya Jumatano ya Majivu, iliyofanyika katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph, mjini Zanzibar juzi jioni. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Waziri aliyetemwa uwaziri na Dk. Shein atoa ya moyoni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Khalid Salum Muhammed, amesema kuwa mabadiliko ya uongozi katika serikali ni jambo la kawaida.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya wizara hiyo na Waziri mpya wa Fedha aliyeteuliwa hivi karibu, Dk. Khalid alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Mohammed Shein kwa kumpa dhamana ya kuiongoza wizara hiyo kwa muda wa miaka mitatu.

Alisema kuwa ushirikiano alioupata kutoka kwa watendaji wa wizara hiyo umempa faraja.

Alieleza kuwa mafanikio hayo ni juhudi za pamoja za watendaji wa wizara hiyo pamoja na miongozo sahihi na kuwataka watendaji kumpa ushirikiano huo waziri huyo mpya. "Nimshukuru kwa dhati Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein kwanza kwa kuniteuwa na kuniamini katika kipindi chote cha miaka mitatu, amenipa maelekezo mengi, nimesoma na nimejifunza mambo mengi kutoka kwake," alisema.

Dk. Khalid pia alimkabidhi ripoti ya wizara hiyo, waziri huyo ambapo inamambo mbalimbali ikiwamo miradi inayosimamiwa na wizara hiyo.

"Waziri huyo siyo mgeni katika shughuli za serikali kwa kuwa ameshawahi kufanya kazi nyingi, hivyo uzoefu wake na ujuzi alionao ninaamini kuwa wizara itaendelea kupata mafanikio makubwa," alisema. Naye Waziri huyo mpya wa Fedha na Mipango, Muhamed Ramia, alisema kuwa mabadiliko hayo yasizushe maswali wala minong'ono kwa kuwa ni jambo la kawaida katika serikali.

Alisema mabadiliko hayo aliyoyafanya Rais ni kwa ajili ya kupatikana ufanisi wa kazi ikiwamo kuongeza kasi ya mapato ambayo ndio muhimu kuendesha serikali.

Alimtaka waziri aliyepita kumpa ushirikiano wa kina hasa ikizingatiwa kuwa kipindi hiki ni cha kuelekea katika bajeti kuu ya serikali ambayo mambo mengi anayafahamu.

# Kabaka awasihi wanawake kuendelea kuonyesha njia

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT), Gaudencia Kabaka, amewataka wanachama wa CCM kisiwani Pemba, kuendelea kuonyesha njia za mafanikio kwa kubuni na kuanzisha miradi endelevu ya kuisaidia jamii.

Aliyasema hayo kisiwani humo akiwa katika ziara zake za kujitambulisha na kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM katika miradi inayotekelewa na UWT pamoja na CCM kwa ujumla.

Akizungumza baada ya kushiriki ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kangagani Wete, Gaudencia alieleza kuwa CCM imekuwa ni taasisi bora ya kisiasa inayotekeleza miradi endelevu inayogusa maisha ya wananchi wa ngazi zote katika jamii.

Alisema kitendo cha wana CCM kujitolea kujenga madarasa ya Shule ya Sekondari Kangagani ni hatua kubwa inayochochea maendeleo ya elimu Zanzibar.

Mwenyekiti huyo alisema maamuzi ya wananchi hao ya kujenga shule hiyo ambayo wanafunzi watapa elimu bora yataendana na hadhi ya serikali.

Gaudensia alisema CCM imeendelea kupiga hatua kubwa ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii kwa lengo la kutekeleza kwa ufanisi ahadi zilizotolewa katika kampeni za uchaguzi mkuu uliopita.

"CCM tunaendelea kutekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020 Zanzibar na Tanzania Bara ili kila mwananchi anufaike na fursa mbalimbali zinazoasisiwa na serikali zote mbili," alisema.

Alieleza kuwa wanawake wanatakiwa kuwa mfano bora wa kufanya kazi kwa kujiamini ili kujikwamua kiuchumi.

Gaudensia pia alitembelea nyumba ya kuwatunza wazee katika kijiji cha Dimbani Pemba na kusema kuwa CCM inathamini na kuwaenzi wazee ambao ndio chimbuko la maendeleo ya nchi.

Alisema wazee wamefanya kazi kubwa ya kujenga maendeleo ya nchi katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii, hivyo lazima watunzwe na kuishi katika mazingira bora.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia idara ya wazee na ustawi wa jamii kwa kuwatunza wazee na kuwapatia huduma zote muhimu.

Naye Makamu Mwenyekiti wa UWT, Thuwaiba Kisasi, alisema kuwa wanawake wanaendelea kujitokeza kwa wingi katika masuala mbalimbali ya kuimarisha chama na jumuiya zake.

# Mtunzi wa riwaya atoa neno kuhusu uandishi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MTUNZI wa riwaya ambaye amenyakuwa Tuzo ya Fasihi ya Afrika ya Mabati Cornnell mwaka 2018, Zainab Bahroun, amesema kuwa uandishi wa riwaya hautaki haraka ili kuhakikisha kazi inakuwa nzuri.

Akizungumza na Nipashe mwandishi huyo wa vitabu, alisema kuwa katika uandishi wa riwaya lazima uwe na nidhamu na kutenga muda maalum kwa ajili ya uandishi.

"Kazi ya riwaya siyo kazi nyepesi lazima utenge muda ili kuweza kukamilisha kile ambacho unataka kukiandika," alisema.

Alisema riwaya yake iliyoshinda katika tunzo hiyo ni Mungu hakopeshwi ambayo inazungumzia matabaka ya watu wenye asili ya Asia na Tanzania.

Alieleza kuwa matarajio yake ni kuipaisha ndoto za mwanamke na kuona mabadiliko katika jamii na heshima na thamani ya mwanamke inaonekana.

Aliwataka wanawake wenye uwezo wa kuandika vitabu ni vyema kuandika ili kuweza kuwasemea wale ambao hawana sauti na kuweza kuibua changamoto zilizopo katika jamii.

"Licha ya kuwasemea wasio na sauti lakini pia kuandika vitabu ili kuweza kudai haki za wanawake ambazo nyingi zimekuwa zikivunjwa," alisema.

Alieleza kuwa bado thamani ya wanamke ipo chini katika jamii na jambo lolote analofanya mwanamke linaonekana kama mazoea bila ya kujali umuhimu wao.

Aidha, alieleza kuwa anafarijika kupokea Tuzo ya ushindi wa Fasihi ya Afrika ya Mabati Cornnell mwaka 2018, kwa kuwa amejifunza mambo mengi kupitia ushindi huo.

Alieleza kuwa hivi sasa anampango wa kuandika kitabu kinachoelezea mbinu mbalimbali za mwanamke kujinasua kutoka kwenye umaskini na kuweza kudai haki ili kuepukana na manyanyaso.

# Wachumi waonya athari za mgomo JKIA

**NAIROBI, Kenya**

MGOMO wa wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) uliopo mjini Nairobi nchini Kenya, huenda ukaleta athari za kiuchumi kwa wakati ujao, hivyo wachambuzi wa masuala ya kiuchumi wataka utafutwe ufumbuzi wa kudumu.

Mmoja wa wachambuzi wa masuala ya uchumi nchini Kenya, Tony Watimu alieleza kuwa ingawa kwa sasa hakuna hasara kubwa za kiuchumi zilizotokea lakini serikali inapaswa kuchukua hatua zinazofaa kumaliza mzozo huo.

"Hatuwezi kusema mzozo hauna madhara makubwa kwa uchumi wa kenya. Serikali ingechukua jukumu kuzungumza na wafanyakazi wanaofanya mgomo ili kutatua mzozo. Kutumia nguvu si njia nzuri ya kusuluhisha mzozo wa kikazi". Alisema Watima.

Maelfu ya wasafiri wa ndege waliokuwa wakisafiri maeneo tofauti duniani kupitia uwanja wa JKIA walipata wakati mgumu juzi baada ya wafanyakazi wa uwanja huo kugoma.

Dakika chache baadaye, Jeshi la Polisi liliwasili na kuwatawanya wafanyakazi hao kwa kutumia mabomu ya kutoa machozi huku baadhi yao na hata wasafiri wakipata majeraha madogo katika purukushani hiyo.

Kiongozi wa wafanyakazi hao, Moss Ndiema alikamatwa na baadaye alifikishwa mahakamani kwa kosa la kuongoza mgomo usio halali, kwani mahakama ilikuwa imetoa uamuzi usitishwe.

Saa sita baadae, idadi kubwa ya wasafiri walikua hawajapata suluhu kwa sababu safari nyingi zilikuwa zimefutwa ama kucheleweshwa. Wengine walipelekwa katika hoteli mbali mbali wasijue hatma yao.

Hata hivyo, baadhi ya wasafiri walipata afueni baada ya wanajeshi wa anga wa KDF kuletwa ili kusaidia katika ukaguzi.

Afisa Mkuu Mtendaji wa KQ, Sebastian Mikos, akizunngumza kwa niaba ya Shirika la Ndege la Kenya alisema safari 24 za ndege zimeathirika kutokana na mgomo huo.

"Tumekuwa tukiwasiliana na wafanyakazi wote wa KAA tangu saa kumi asubuhi, kwa kweli ni shughuli katika uwanja wa JKIA na viwanja vengine nchini zimeathirika kutokana na mgomo huu kwa wakati huu tutasema kwamba safari za ndege zimechelewa... safari za ndege 24 zimeathirika" Alisema Mikos na kuongeza

"Wakuu wengine wa Kampuni za ndege huenda wamechukua maamuzi tofauti kwa kutua katika viwanja vingine au kusitisha safari".

Katika mgomo huo walioathirika zaidi ni abiria ambao walikwama kwa saa kadhaa.

*BBC*



Wafanyakazi wa Shirika la Ndege la Kenya wakitawanywa na askari wa kikosi cha kuzuia ghasia katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa-Jomo Kenyatta, Nairobi. **PICHA: REUTERS**

## Kampuni ya kutengeneza simu yaishtaki Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

KAMPUNI ya kutengeneza simu ya Huawei imeishtaki serikali ya Marekani ikipinga sheria iliyoipitisha mwaka jana inayokataza taasisi za serikali za Marekani kununua bidhaa za Huawei.

Mwenyekiti wa Huawei, Guo Ping alisema kwamba wamelazimika kwenda mahakamani kwa sababu Marekani imeshindwa kutoa uthibitisho wa kuonyesha haja ya kuweka marufuku hiyo ambayo inaweza kuwatoa katika ushindani wa kibiashara wa huduma ya kasi ya mtandao wa 5G.

Kesi hiyo iliwasilishwa katika mahakama iliyopo katika Jimbo la Texas inakipinga kipengee cha 889 katika kifungu cha sheria za mamlaka ya usalama wa taifa wa Marekani iliyotiwa saini Agosti mwaka jana na Rais wa Marekani, Donald Trump.

Sheria hiyo imezikataza taasisi za serikali ya Marekani pamoja na wakandarasi wake kununua vifaa au huduma za kampuni ya Huawei. Guo alisema katika kesi hiyo pia watadai fidia kutokana na hasara mbali mbali zinazojiri kutokana na sheria hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya kampuni hiyo yaliyopo mji wa Shenzhen, Kusini mwa China, Guo alisema Marekani inatumia kila mbinu kuipaka tope kampuni ya Huawei. Alisema Marekani pia imedukua mitambo mikuu ya kampuni hiyo na kuiba barua pepe na vyanzo vya kodi zao.

Ni muda mrefu sasa Marekani imekuwa ikiamini kwamba kampuni ya Huawei ni tishio kwa usalama wake hasa kwa kuzingatia mwanzilishi wa kampuni hiyo, Ren Zhengfei alikuwa mwandisi wa Jeshi la China.

Hofu ya Marekani imezidi baada ya kampuni hiyo kupanuka zaidi ulimwenguni na kuongoza katika vifaa vya mawasiliano vinavyounganisha sehemu kubwa ya mataifa ulimwenguni.

Vilevile, Huawei ni mojawapo ya kampuni kubwa zinazotengeneza simu za kisasa.

Marekani imeonya kwamba vifaa vya Huawei vinaweza kutumiwa na serikali ya China kuyapeleleza mataifa mengine na kuharibu mawasiliano muhimu hivyo kuyataka mataifa kuisusia kampuni hiyo.

Kwa upande wake Huawei imesema kampuni hiyo iliyo na matawi katika nchi 170 haijawahi kushiriki katika uvunjaji wa sheria zozote za kiusalama na pia haijawahi kupokea maombi kutoka kwa serikali ya China kuweka vifaa vya siri kuiwezesha kufanya ujasusi.

**DW**

## Tshidekedi, Kabila watangaza serikali ya muungano

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi na mtangulizi wake Rais Joseph Kabila, wameamua kuunda serikali ya muungano baada ya mazungumzo.

Licha ya kutangazwa kuwa mshindi katika uchaguzi uliofanyika Desemba mwaka jana, Rais Tshisekedi amejikuta akilazimika kugawanya uongozi.

Lakini hadi sasa Rais Tshisekedi hajafanikiwa kumteua Waziri Mkuu kutokana na muungano wa Common Front for Congo (FCC) kuwa na idadi kubwa ya wabunge.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, Rais Tshisekedi na Kabila walisema: "licha ya FCC kuwa na wingi wa wabunge na katika kuidhinisha matakwa yalioelezewa na wapiga kura, FCC na CACH wanaonesha uwajibikaji wa malengo yao ya kuongoza pamoja kama sehemu ya serikali ya muungano".

Kwa miaka 18 DRC taifa lenye utajiri wa madini limeongozwa na Rais Joseph Kabila, hivyo kuwania urais kwa Tshisekedi kulionekana kama ndoto za kumpindua Rais Kabila.

Vilevile, baadhi ya wachambuzi walieleza kuwa Tshisekedi hajawahi kushikilia wadhifa wowote wa juu au kuwa na uzoefu wa usimamizi.

Lakini kadri muda ulivyosogea Rais Tshisekedi amefanikiwa kupanda cheo, kuanzia mwaka 2008 ambapo alikuwa katibu wa taifa aliyeangazia masuala ya uhusiano wa nje. Aliteuliwa kuwa kiongozi wa chama cha UDPS baada ya kifo cha babake Etienne Tshisekedi.

Rais Tshisekedi, ambaye haungwi mkono sana kama ilivyokuwa kwa baba yake, mwaka jana alisema kwamba akishinda urais atаunda tume ya ukweli, haki na maridhiano na kumuwajibisha Rais Kabila. Lakini atamruhusu kusalia nchini Congo.

Changamoto kubwa iliyopo kwa sasa ni namna gani Rais Tshisekedi anaweza kuleta amani na maridhiano kwa taifa hilo hususani eneo la mashariki ambako kumekuwa na ghasia na umwagikaji damu kwa raia, na uwapo wa wanamgambo waliojihami wanaotekeleza mashambulio.

*BBC*



Meneja Mawasiliano na Matukio wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Christina Murimi (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi wa kituo cha Mwanangu Special, Walter Miya, vifaa vya watoto wenye mahitaji maalumu kutoka taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation. Anayeshuhudia makabidhiano hayo ni Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nderemo, vifijo Mbowe kuachiwa kwa dhamana

INATOKA UK 2

kuwa ni kama kesi inadhaminika, kutoa dhamana ni tafsiri dhahiri ya mahakama ya dhana ya katiba ya kuwa mtu hana hatia mpaka mahakama itakapomhukumu vinginevyo, kufuta dhamana kunahitaji sababu kubwa kuliko sababu za kumpa mtu dhamana, na mahakama izingatie ukubwa wa kosa kutoa masharti ya dhamana.

Vingine ni masharti ya dhamana yawekwe bila kuleta hisia kuwa mpango ni kumnyima mtu dhamana, mahakama izingatie adhabu kwa makosa yaliyopo mbele yake ili pale mshtakiwa akitiwa hatiani asiwe amedhibitiwa mara mbili, sababu ziwe zinakubalika na mahakama yoyote duniani, mahakama izingatie msongamano uliopo gerezani na je, kutoa dhamana au kufuta dhamana kunachangia au kupunguza msongamano gerezani, na mwisho mahakama izingatie kuwa uhuru wa mshtakiwa hauna mbadala.

Mapema wiki iliyopita Mahakama ya Rufani ilitupilia mbali rufani ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) ya kupinga Mbowe na mwenzake kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Mbowe na Matiko wote kwa pamoja wamekata rufani wakipinga kutenguliwa kwa dhamana yao na Hakimu Mkazi Mkuu, (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu) Wilbard Mashauri.

Katika maombi yao, walalamikaji wanadai kwamba Mahakama ya Kisutu ilikosea kufuta dhamana kwa washtakiwa wakati wao wenyewe walifika mahakamani Novemba 12. Pia walihudhuria mahakamani Novemba 23, mwaka jana siku dhamana yao ilipofutwa.

Novemba 23, Mahakama ya Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mashauri iliwafutia dhamana Mbowe na Matiko baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yao ilipopangwa kati ya Novemba Mosi na 8, mwaka jana.

Katika kuifuta dhamana hiyo, Mashauri alisema Novemba Mosi, mdhamini wa Mbowe alidai mahakamani kwamba mshtakiwa ameugua gafla yuko mahututi hawezi kuzungumza na amepelekwa kutibiwa nje ya nchi.

Pia Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai kuwa mshtakiwa ni mgonjwa mahututi amepelekwa nchini Afrika Kusini.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alipinga sababu zilizotolewa na utetezi na kuiomba mahakama kuuamuru utetezi kuwasilisha vielelezo kuhusu maradhi ya Mbowe.

Mahakama iliamuru washtakiwa wakamatwe na kufikishwa mahakamani kujieleza kwanini wasifutiwe dhamana, lakini Novemba 12, Mbowe na Matiko walijisalimisha mahakamani.

Mbowe wakati akijitetea ili asifutiwe dhamana alidai kuwa aliondoka nchini Oktoba 28, mwaka jana kwenda Marekani na alianza kuugua akiwa huko Oktoba 31.

Alidai kuwa Novemba 2, alikwenda nchini Ubelgiji wakati akisubiri ahadi ya kuonana na daktari wake Novemba 8 na kwamba alishauriwa asisafiri mwendo mrefu akiwa angani.

Kwa upande wake, Matiko alidai kuwa alishindwa kufika mahakamani kwa sababu alihudhuria mkutano wa michezo kwa mabunge ya Afrika Mashariki akiiwakirisha Tanzania.

"Kwa kuwa mshtakiwa wa kwanza taarifa zake zinakinzana, hati yake ya kusafiria inatofautiana na maelezo yake, mshtakiwa wa tano pia sababu zake hazina mashiko, mahakama yangu inawafutia dhamana kuanzia leo," alisema Hakimu Mashauri.

"Nchi yetu inaendeshwa kwa matakwa ya sheria, pamoja na nyadhifa walizonazo mshtakiwa wa kwanza na wa pili, wanakabiliwa na makosa ya jinai wanapaswa kutii amri za kisheria," alisema hakimu na kuongeza.

Katika kesi ya msingi, mbali na Mbowe na Matiko, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; na Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji wa kosa la jinai kati ya Februari 1 na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam.

## Kigwangalla aweka msimamo mapambano dhidi ya ujangili

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, amewataka Watanzania kuondokana na dhana iliyojengeka miongoni mwao kuwa watumishi wa wizara hiyo husuan wahifadhi wa wanyamapori na misitu ni wakatili wanaowatesa wananchi.

Kigwangalla alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa 26 wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo, uliofanyika katika Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi, jijini Mwanza.

Alisema watumishi hao ni watu wenye utu na weledi wa hali ya juu na wanaozingatia sheria katika kutimiza majukumu yao.

Hata hivyo, Waziri Kigwangalla alisema wafanyakazi hao hulazimika kutumia nguvu wakati wakipambana na watu wanaokutwa katika maeneo ya hifadhi wakifanya vitendo vya ujangili.

"Ulinzi wa rasilimali za nchi ni jukumu letu sote. Wizara imepewa dhamana ya kusimamia na kuongoza kwa niaba ya Watanzania. Kama kuna watumishi wa wizara hii wanaowanyanyasa wananchi, naomba walete ushahidi ili tuwachukulie hatua," alisema.

Waziri Kigwangalla alielezea kusikitishwa na idadi ya watumishi walipoteza maisha kwa ajali na wengine kuuawa na majangili wakati wakipambana nao katika maeneo ya hifadhi na kutoa wito kwa wananchi wote wenye taarifa au ushahidi juu ya vitendo vyovyote vya kihalifu, kuziwasilisha katika mamlaka husika.

Alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua watu wanaojihusisha na vitendo vya ujangili na uhalifu katika maeneo ya hifadhi pamoja na wanaoshirikiana na makundi ya watu wenye nia ovu ya kukwamisha juhudi za uhifadhi wa rasilimali za taifa.

Dk. Kigwangalla aliwataka wananchi kuheshimu sheria za uhifadhi na kuepuka kuvamia maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kijamii na ufugaji.

Sambamba na hilo, alitoa wito kwa viongozi wa siasa kuunga mkono juhudi za wizara katika ulinzi wa maeneo ya hifadhi kwa kuwaelimisha wananchi wanaowaongoza kujiepusha na vitendo vya uvamizi wa maeneo ya hifadhi badala ya kuwatetea.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, alisema watumishi 23 walifariki dunia wakati wakitekeleza majukumu ya uhifadhi na watano walijeruhiwa na majangili wakiwa kazini.

Prof. Mkenda alisema kuwa waliofanya vitendo hivyo hawaitakii mema Tanzania na ni maadui wa uhifadhi na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kusimama na kuwatetea watumishi na askari wa wanyamapori wanaotimiza majukumu yao kwa kuzingatia sheria.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



## CHETI KIMEPOTEA



**OBADIA K. ZABRONI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Taaluma ya Ualimu Daraja la Kwanza kilichotolewa na Baraza la Mtihani Taifa chenye **index namba E.0601-0023** Kinondoni Muslim mwaka 2015. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **MAG/RB/8696/2017.**

115101902

## KUPOTEA KWA KWA CHETI



**James Dotto** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2968-0035** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Lagangabilili.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **BAR/RB/1754/2018**

115101402

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**MORGAN SAMWEL MARUNDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina M/DION yenye namba za usajili T 173BKB. Chassis CR61WOO1601 Engine Namba 4GD41MR9022.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/2650/2018.**

115102201

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CRISPER MAKELWA SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba **MC 935 BRW** aina ya Bajaj Boxer yenye chassis namba **MD2A21BYOHWA56274** na,engine namba **PF2WHA11215.** Yeyote atakaeiona atoe taaarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.Taarifa ya polisi **KJN/BI/I/VOL/3448/2019**

115102002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;60/2019**


**Ombi la AGNES BONIFASI NJOHOLE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BONIFASI YUSTINI NJOHOLE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 06/03/2019.

XXXXXXX

## CHETI KIMEPOTEA



**HOTAY NEEMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha UALIMU chenye **index namba E.529/57** kilichotolewa na chuo cha TARIME mwaka 1981. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1397/2019**

115101302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MARY DERECK BARUBUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya TOYOTA CORONA yenye namba za usajili T839 BSW. chasis na. AT2100008505, Engen na.4AL272902

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **KJN/RB/1344**

115101202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 07/03/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 09/03/2019 kampuni ya M.E Company Ltd itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar kuelekea Morogoro gari hilo lenye namba za usajili:

   **T802 Horse/Horse/T 812 AKE Trailer.**

2. Garihilolinavipimovifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 2.80**
   **Kimo - mita 4.80**

3. NJia itakayotumika Morogoro hadi Dar es Salaam kupitia Kilwa Road gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

115101502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 07/03/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 09/03/2019 kampuni ya M.M Corporate Ltd itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar kuelekea Mkuranga gari hilo lenye namba za usajili:

   **T898 APY Horse/T 933 AFZ Trailer.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 2.80**
   **Kimo - mita 4.80**

3. NJia itakayotumika Dar hadi Mkuranga kupitia Kilwa Road gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

115101102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA DODOD**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 36 YA 2018**
**BAINA YA:**
**MUOMBAJI...............................JOYCE MAZENGO**
**DHIDI YA**
**WADAIWA.................................JUMA A. SUME**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA KUWA** Muombaji ameleta maombi yake ambayo yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo yanapatikana katika baraza hili.

**KWA HIYO** unahitajika kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye ameruhusiwa kisheria tarehe 11.03.2019 saa tatu asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** Kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza litadhibitisha kama umepokea Hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 05/3/2019.

115102302


## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MBAPPE

## KUMBADILI BALE MADRID

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid imepanga kumuunganisha, Kylian Mbappe, katika kikosi chake kwenye msimu huu wa kiangazi endapo itapata upenyo wa kuachana na Gareth Bale, kwa mujibu wa Don Balon.

Madrid imekuwa na kiu ya kumnyakua Mbappe anayetazamwa kama Cristiano Ronaldo au Lionel Messi wa siku za usoni, lakini mtihani mkubwa ni uwepo wa Bale na kitita anachotaka kwenye timu hiyo.

Inaelezwa kuwa Bale yuko mguu pande na mguu sawa kutaka kuachana na Real Madrid wakati wowote hali inayompa nafasi zaidi Mbappe kupenya kwenye kikosi hicho.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United na Tottenham, Drimitiv Berbatov amemshauri Bale kuachana na Real Madrid kutokana na hali inayoonekana hivi sasa ya kulaumiwa kwa kila kipigo wanachopata.

"Bale anaonekana kulaumiwa kwa kila kitu kinachoenda vibaya ndani ya Real Madrid, kitu ambacho sio sahihi.

"Katika msimu huu amepata magoli 12 kwenye michezo 30, anafanya vizuri lakini bado analaumiwa. Kama unajisikia haukubaliki, unapaswa kuondoka," alisema Berbatov alipofanya mahojiano maalum na Betfair.

"Ni suala la fedha tu, sidhani kama Tottenham wana uwezo wa kulipa mamia ya mamilioni ya dola kwa mchezaji mmoja. Lakini Bale ni mchezaji wa kiwango cha juu duniani na itakuwa vizuri kwake kurejea kwenye Ligi Kuu," aliongeza.

Robert Pires alimtaja Mbappe kuwa mchezaji ambaye ana nafasi ya kushinda Ballon d'Or siku za usoni.

## MULLER AMJIA JUU KOCHA UJERUMANI

**MUNICH, Ujerumani**

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Thomas Müller, amemshutumu kocha wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low, kupitia mitandao ya kijamii, baada ya kumwacha katika kikosi chake hicho pamoja na Jérome Boateng na Mats Hummels.

Baada ya kuwa na matokeo mabaya kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana na pia kushindwa kutamba kwenye Ligi ya Mataifa ya Ulaya, Low ameamua kukipangua kikosi chake wakati akielekea kwenye michuano ya kufuzu Euro 2020 dhidi ya Serbia na Uholanzi mwezi ujao.

Muller alionekana kutofurahia kuachwa kwenye kikosi hicho na haraka aliamua kuonyesha hisia zake kupitia mitandao ya kijamii.

Katika ujumbe wake alioandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 aliandika: "Nimelala na kuacha maamuzi yaliyofanywa.

"Nilichanganywa na uamuzi wa jana (juzi) juu ya kocha kuamua kuniacha timu ya taifa. Ameamua kuchukua uamuzi sahihi. Hata hivyo, siwezi kumuuliza.

"Hata hivyo, siwezi kulifikiria zaidi hilo, lakini jinsi jambo lenyewe lilivyokwenda limenifanya nijisikie vibaya.

"Naelewa ni uamuzi wa kocha mwenyewe, Mats, Jerome, na mimi bado tunauwezo wa kucheza soka katika kiwango cha juu kabisa. Tuna safari ndefu ya kwenda."



## Juventus kumrudisha Conte

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus inaaminika kwamba inataka kumleta tena Antonio Conte kuwa kocha wa timu hiyo msimu ujao, huku nyota wa zamani Andrea Pirlo akijiunga kama kocha msaidizi.

Conte alitumia muda mwingi wa uchezaji wake akiwa na klabu hiyo na alirudi kuwa kocha wa kikosi hicho mwaka 2011.

Akiwa na timu hiyo alikuwa na mafanikio makubwa, baada ya kufanikiwa kuipa mataji matatu mfululizo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Baada ya kuwa na mafanikio makubwa katika klabu za Juve na AC Milan, Pirlo alistaafu kucheza soka mwaka 2017, na sasa anaonekana kuwa tayari kuanza kazi ya ukocha.

Kwa mujibu wa Tuttosport, Juventus inahisi kwamba Conte ndiye anayefaa kuchukua mikoba ya Massimiliano Allegri wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, kocha huyo wa zamani wa Chelsea kwa sasa hana kazi yoyote na kwamba anaweza kukubali haraka kuchukua mikoba hiyo na kuinoa Juve.



## HABARI MICHEZO



# Lukaku:
## Solskjaer atabakia United

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Romelu Lukaku, amebainisha hana shaka kuwa, Ole Gunner Solskjaer atateuliwa kuwa kocha wa kudumu baada ya kuiwezesha timu hiyo kupindua matokeo na kuifunga Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora na kutinga robo fainali.

United waliingia kwenye mchezo huo wakiwa nyuma kwa mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza mwezi uliopita na waliachwa wakitakiwa kupanda mlima mkubwa katika mchezo huo wa pili, huku pia wakiwa na wachezaji 10 majeruhi.

Lakini mabao mawili ya Lukaku na lile la penalti la Marcus Rashford yaliiwezesha kuibuka na ushindi wa 3-1 na kufuzu kwa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

United sasa imeshinda mechi 14 kati ya 17 tangu Solskjaer alipoteuliwa kuwa kocha wa muda, ikiwamo rekodi ya asilimia 100% ya kushinda mechi za ugenini.

Na sasa Lukaku amesema kuwa Solskjaer ana nafasi kubwa ya kupewa mkataba wa kudumu wa kuwa kocha wa timu hiyo.

"Najua kwamba atabakia, hakuna shaka na hilo," amesema akiiambia televisheni ya Viasport.

"Anataka kubakia hapa, wachezaji wanamtaka yeye kubakia hapa. Tunafanya vizuri kama ambavyo Manchester United wanatakiwa kucheza. Ni kocha kijana, akiwa na wachezaji vijana na kuna mazingira mazuri hapa.

"Mara zote ni suala la kujiamini. Wakati ukiangalia timu yetu, tuna wachezaji wengi wenye kujiamini, lakini anatuambia maneno mazuri katika wakati muhimu.

"Ndio maana unahitaji wachezaji vijana, wakati mwingine unahitaji kuimarika zaidi, lakini kuna wakati unahitaji kujiimarisha zaidi."

Mchezo unafuata wa Solskjaer kwa United, itakuwa dhidi ya Arsenal Jumapili na wakiwa kwenye mbio za kuwania nafasi nne za juu.

## LUIZ: WACHEZAJI CHELSEA WANA IMANI NA SARRI



**LONDON, England**

BEKI wa Chelsea, David Luiz, amesisitiza kuwa kila mchezaji katika klabu hiyo ana imani na falsafa ya kocha, Maurizio Sarri na kwamba kila anachokifanya kwa asilimia 100% wanakiunga mkono hapo Stamford Bridge.

Sarri alileta mfumo wa 'Sarri-ball' hapo Chelsea, mfumo ambao aliutumia kwenye klabu yake ya zamani ya Napoli, lakini imeshindwa kufanya kazi.

"Ni kuhusu kile tunachokiamini. Kila mchezaji anaamini katika falsafa yake na kila mmoja ana imani nae kwa asilimia 100%," amesema Luiz akiiambia BBC Sport.

"Tuliishi kwenye wiki chache ngumu na wachezaji wameweza kuzoea haraka. Kocha amezoea haraka, na wachezaji pia wameweza kuifahamu falsafa yake," aliongeza mchezaji huyo raia wa Brazil.

"Ulikuwa ni uamuzi wa klabu kubadilisha staili ya uchezaji wa soka. Kwa miaka mingi watu walikuwa wanasema Chelsea walikuwa wanashinda, lakini tulishindwa kutawala mchezo.

"Lakini sasa tunatawala mchezo na watu wanasema hatushindi."

Chelsea ilikumbana na kichapo cha 4-0 kutoka kwa Bournemouth Januari, kabla ya kukutana na dhahama ya kufungwa 6-0 na Manchester City mwezi uliopita.

Na hiyo ikachangia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa uvumi kwamba, kocha huyo raia wa Italia anaweza kutimuliwa wakati wowote.

"Ni mtu mwenye utu, mtu mwenye mapenzi na soka anawapenda watu na anajaribu kwa hali na mali kuhakikisha timu inafanya vizuri," amesema Luiz.

"Wakati unapopoteza mchezo, kama tulivyofanya dhidi ya Manchester, hakuna mtu ambaye anaweza kufurahia matokeo mabaya. Yeye ni mtu ambaye anaonyesha jambo linalomuumiza."



## Solskjaer: Hii ndio Manchester United

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kwamba walichokifanya jijini Paris kwa kuifunga PSG kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, ndio kitu wanachokifanya.

Lukaku alifunga mabao mawili kabla ya penalti ya Marcus Rashford iliyotolewa kwa mfumo wa VAR kuiwezesha United kufuzu kwa robo fainali ya michuano hiyo.

"Ni klabu hii. Ndicho tunachokifanya, hii ndio Manchester United," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

Solskjaer alifunga bao la dakika ya mwisho kwa timu hiyo katika fainali ya michuano hiyo mwaka 1999.

Hii ni mara ya kwanza tangu mwaka 2014 ambapo United imefuzu katika hatua ya robo fainali. Timu za mwisho zitakazofuzu kwa robo fainali zitajulikana Machi 12 na 13, huku droo ikitarajiwa kupangwa Machi 15 mwaka huu.

"Tunaweza kwenda mpaka mwisho," amesema Solskjaer. "Ndio tunajipendelea, lakini inabidi tusubiri droo halafu tucheze mchezo namna unavyokuja."

Raia huyo wa Norway ameongeza: "Ni usiku wa kawaida kwa Manchester United. Tulikuwa na mpango wa mchezo na imani kwa wachezaji ndiyo tulioitarajia. Kila mtu anahisi fahari kubwa."

Bao la utangulizi la Lukaku liliipatia United matumaini na licha ya kwamba Juan Bernat wa PSG alilisawazisha, Lukaku alifunga tena bao jingine katika nusu ya kwanza ya mechi kabla ya Rashford kuifunga siku kwa ushindi wa mashetani hao wekundu.

"Ulikuwa ni mwanzo mzuri - tulipanga kufunga bao la kwanza, lakini hatukulitarajia baada ya dakika mbili za kuanza mechi," alisema Solskjaer. "Tuliona katika mechi baina ya Real Madrid na Ajax, Barcelona dhidi ya PSG [mnamo 2017] - kuna hali ambazo zinafanana na inaonyesha kwamba akili ni muhimu katika soka.

"Vijana wetu ni wadogo na wenye umahiri, na ndicho kilichotupatia ari na nguvu wakati tulipolihitaji bao."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED KUMTANGAZA SOLSKJAER MAPEMA

Wachezaji wakongwe wamkubali mshambuliaji huyo wa zamani wa timu hiyo...

**MANCHESTER, England**

WACHEZAJI wa Manchester United wanatarajia Ole Gunnar Solskjaer atatangazwa rasmi kuwa kocha wa kudumu wa klabu hiyo kabla ya mwisho wa msimu huu, ikiwa ni muda mchache baada ya kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Taarifa za ndani zimeiambia ESPN FC kuwa watendaji wakongwe wa Old Trafford sasa wanajiandaa kusikia taarifa ya Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward kuthibitisha kuwa kocha huyo raia wa Norway ndio mrithi rasmi wa Jose Mourinho.

Solskjaer ameiongoza United kupata ushindi katika mechi 14 kati ya 17 akiwa kaimu kocha na juzi Jumatano alifanikiwa kupata ushindi wa mabao 3-1 ugenini dhidi ya Paris Saint-Germain katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ushindi huo wa ugenini umeifanya United kupindua matokeo baada ya kufungwa magoli 2-0 katika mechi ya kwanza na kuipeleka timu hiyo kwenye hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ikiwa ni mara ya kwanza kufika hatua hiyo tangu msimu wa 2013/14.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 46 amekuwa na mafanikio tangu alipochukua mikoba ya Mourinho, Desemba, mwaka jana na vilevile amempiku Kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, ambaye alikuwa akipewa nafasi ya kwanza ya Woodward kuchukua nafasi hiyo.

Klabu hiyo inaendelea kusisitiza kuwa nafasi hiyo ya kocha itatangazwa ifikapo mwishoni mwa msimu huu, lakini tayari kumekuwa na matumaini ndani ya kikosi chao na mtu anayeweza kupewa madaraka kutangazwa kabla ya Mei mwaka huu.

ESPN FC iliripoti kuwa mpaka sasa United bado haijafanya mazungumzo na kocha yoyote kuhusu kumpa mkataba wa kudumu ndani ya klabu hiyo ya Old Trafford, zaidi ya Solskjaer, ambaye anatarajiwa kuthibitishwa hivi karibuni badala ya hapo baadaye kama ilivyokuwa inajulikana.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa United, ambaye ametua kwenye timu hiyo baada ya kuazimwa kwa mkopo akitokea kwenye klabu ya Molde ya Norway tayari ameshaanza mipango ya ziara ya maandalizi ya msimu mpya ya kipindi cha majira ya joto kwa kupendekeza kikosi hicho kiende Australia na Mashariki ya mbali.

Na Solskjaer pia alikuwa ameruhusiwa kujihusisha na mipango ya usajili na mahitaji yake ya kuboresha kikosi hicho kwa baraka za Woodward, huku pia akikubali kumuuza Marouane Fellaini kwenda katika klabu ya Shandong Luneng ya China mapema Januari mwaka huu.

Ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo, Solskjaer amekuwa ni mtu muhimu baada ya kuwapo na hofu wakati wa kipindi cha utawala wa Mourinho. Na baada ya ushindi dhidi ya PSG, Solskjaer ameanza kupigiwa debe na wachezaji wakongwe wa timu hiyo.

"Najua ataendelea kubakia hapa, hakuna shaka kuhusu hilo," alisema Romelu Lukaku. "Anataka kubaki, wachezaji wanamhitaji abakie.

"Ni kocha kijana, ana wachezaji vijana ambao wanahitaji kukua na kupata maendeleo na naamini tutashinda mataji huko mbele.

Ashley Young, ambaye alikuwa nahodha wakati United ikiwa jijini Paris, aliongeza kuwa sauti yake imekuwa ikiongeza nguvu katika kikosi chao ambacho kilitoka kwenye changamoto.

## KWA UFUPI

### MOURINHO ANUKIA MADRID
ALIYEKUWA Kocha wa Manchester United, Jose Mourinho, ana asilimia kubwa ya kurejea katika klabu yake ya zamani ya Real Madrid katika kipindi cha majira ya joto, aliondoka klabuni hapo mwaka 2013 na kujiunga na Chelsea. ***(Telegraph)***

### SOLARI CHUPUCHUPU
RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, alitaka kumfukuza kazi kocha Santiago Solari muda mfupi baada ya kufungwa na Ajax katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa Jumanne iliyopita, lakini baada ya kuona hakuna mbadala wa atakayeiongoza timu hiyo hadi mwisho wa msimu aliamua kusitisha uamuzi huo. ***(Marca)***

### PEREZ AVURUGWA
FLORENTINO Perez aliongoza kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wa Real Madrid kilichofanyika kwenye Uwanja wa Bernabeu hadi saa nane usiku baada ya timu yao kufungwa na Ajax. ***(AS)***

### BALE KUKUBALI HASARA
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (29), atalazimika kupoteza kiasi kinachofikia pauni milioni 70 katika mshahara wake kama ataamua kuondoa Real Madrid katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

### KLOPP AIKATAA MADRID
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ataikacha ofa yoyote kutoka Real kwa ajili ya kutua klabuni hapo Bernabeu katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Telegraph)***

### WERNER ANUKIA LIVERPOOL
MABOSI wa Liverpool wameanza mawasiliano na RB Leipzig kwa ajili ya kumsajili straika Mjerumani, Timo Werner (23), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Bild, via Liverpool Echo)***

### ABRAHAM KUTUA LEIPZIG
RB Leipzig inajipanga kumsajili mshambuliaji wa Chelsea ambaye ni raia wa England, Tammy Abraham (21), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Aston Villa. ***(Sun)***

### CONTE KUREJEA JUVE
JUVENTUS inajiandaa kumwajiri kocha wake wa zamani, Antonio Conte na kiungo wa zamani wa Italia, Andrea Pirlo awe msaidizi wake kama kocha, Massimiliano Allegri ataondoka klabuni hapo. ***(Tuttosport - in Italian)***

### SANCHO KUBAKI DORTMUND
WINGA raia wa England, Jadon Sancho (18), anajiandaa kuikacha Manchester United na kubakia Ujerumani katika klabu yake ya Borussia Dortmund. ***(Sun)***

### EVERTON: HOLGATE HAUZWI
EVERTON haina mpango wowote wa kumuuza beki wake wa kati, Mason Holgate, katika kipindi cha majira ya joto licha ya kutakiwa na West Brom ambaye inashiriki Ligi ya Championship, klabu ambayo beki huyo mwenye umri wa miaka 22 anaitumikia kwa mkopo. ***(Liverpool Echo)***

### BARCA: TUNAMTAKA LIGT
RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amethibitisha klabu hiyo inamhitaji beki wa kati wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt (19), ikiwa tayari imeshamsajili mchezaji mwenzake wa timu hiyo, Frenkie de Jong (21). ***(SER, via Independent)***

### BAKAYOKO NJIA PANDA
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Chelsea, Tiemoue Bakayoko (24), amesema hajui hatima yake baada ya kumaliza muda wake wa mkopo katika klabu ya AC Milan kumalizika. ***(France Football - in French)***

## HABARI MICHEZO

# JULIO ASIMAMISHWA, AWADAI DODOMA FC

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA kuwapo kwa taarifa ya kutimuliwa kwa Kocha Mkuu wa Dodoma FC, Jamhuri Kihwelu 'Julio', uongozi wa klabu hiyo umesema kuwa bado wanaendelea kumtambua kocha huyo, lakini kwa sasa wamemsimamisha kazi.

Taarifa ya kutimuliwa Julio zilianza "kuzagaa" juzi kwa madai kuwa uongozi haujaridhishwa na mwenendo wa timu yao inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza hapa nchini.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Johnson Fortunatus, alisema kuwa uongozi wa timu hiyo umekubaliana kulisimamisha benchi la ufundi la klabu yao ambalo liko chini ya Julio kwa muda, wakati Kamati ya Utendaji ikiendelea kujadiliana kwa ajili ya kupata suluhisho la kudumu.

"Tumekubaliana kuwasimamisha, watakuwa nje ya majukumu yao kwa sasa mpaka kamati itakapotoa uamuzi mwingine, napenda kusema kuwa hatujamfukuza, kama uongozi tumekubaliana naye hivyo na kama kuna stahili zake uongozi lazima ukamilishe kabla ya kuachana naye jumla," alisema Fortunanus. Kiongozi huyo alisema kwa sasa hawawezi kutangaza kuwa wamemfukuza Julio zaidi ya kusema wamemsimamisha na jambo hilo ni la kawaida kwa wafanyakazi baada ya kuona kwamba mambo hayaendi sawa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Julio alisema kuwa hana taarifa zozote za kutimuliwa katika timu hiyo na kuongeza kwamba anaidai klabu hiyo.

"Sijatimulia kazi, lakini nami kwa upande wangi nina madai ya msingi kwa uongozi," alisema kwa kifupi beki na kocha huyo wa zamani wa Simba ya jijini Dar es Salaam.

Dodoma FC ina pointi 17 baada ya kucheza mechi 14 na katika msimamo wa Kundi B linaloongozwa na Geita Gold FC yenye pointi 29 baada ya kushuka dimbani mara 14 iko katika nafasi ya nane.




Mwalimu wa Shule ya Atlas ya Madale jijini Dar es Salaam, Renovatus Philbert (kushoto), akikabidhiwa zawadi ya hundi yenye thamani ya Sh. milioni 26.6 baada ya kushinda Multibet ya SportPesa. Kulia ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa SportPesa, Luca Neghesti. **PICHA: SPORTPESA**

# SportPesa yampa nyumba mwalimu

**Na Mwandishi Wetu**

MWALIMU wa Shule ya Atlas iliyoko Madale jijini Dar es Salaam, Renovatus Philbert, amefanikiwa kupata kitita cha Sh. milioni 26.6 baada ya kushinda Multibet ya SportPesa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Philbert, alisema kuwa huo ni ushindi wake wa pili kushinda ndani ya mwezi huu baada ya hivi juzi kushinda Sh. milioni 10.

Philbert ambaye ni mkazi wa Tegeta jijini alisema kuwa baada ya ushindi huo amepanga kuzitumia pesa hizo alizozipata kwa kununua kiwanja na kuanza ujenzi wa nyumba atakayoishi yeye na familia yake.

Aliongeza kuwa huu ni mwaka wa tatu kwake tangu alipoanza kubashiri na SportPesa na kujishindia mara kadhaa fedha baada ya ubashiri wake mzuri aliokuwa akiufanya wa mechi mbalimbali.

**"Kampuni ya SportPesa ni tofauti na nyingine ambazo nilizowahi kucheza nazo, yenyewe ukishinda kwa usahihi katika mechi zako, basi ndani ya dakika ya 10 unatumiwa fedha zako kupitia simu yako ya mkononi.**

"Hivyo, nimepanga kuendelea kubashiri matokeo na SportPesa ambayo nimekuwa nikiiamini katika malipo yao ya fedha baada ya ushindi, hivyo niwashauri vijana wabashiri matokeo na SportPesa," alisema Philbert.

Naye Mkurugenzi wa Uendeshaji wa SportPesa, Luca Neghesti, alimpongeza Philbert kwa ushindi huo wa Multibeti, huku akimtaka kuendelea kubashiri zaidi kupitia SportPesa ili ajishindie pesa zaidi. Wakati huo huo, fundi ujenzi wa Buza, Kanisani jijini, Juma Mililu, naye ameibuka mshindi wa Jackpoti Bonasi baada ya kujishindia Sh. milioni 31.8 baada ya kufanikiwa kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

Mililu alisema baada ya ushindi wa fedha hizo, amepanga kununua kiwanja na haraka ataanza ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi yake.

"Niwashauri vijana wenzangu kubashiri matokeo yao kupitia SportPesa ambayo mimi nilianza kucheza tangu mwaka 2017, hivyo baada ya ushindi huu nimepanga kuendelea kubashiri na SportPesa," alisema Mililu.

## Katiba zachelewesha uchaguzi mkuu ZFA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MCHAKATO wa uchaguzi wa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) utaanza rasmi mwishoni mwa mwezi huu baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa ngazi ya mikoa, imeelezwa.

Awali ZFA ilitangaza kuwa itafanya uchaguzi wake wa kupata viongozi wapya watakaoingia madarakani mwezi uliopita.

Katibu Mkuu wa ZFA, Muhamed Ali Hilali "Tedy", alisema kuwa lengo la kusubiri kumalizika kwa uchaguzi wa mikoa ni kwa ajili ya kupata viongozi watakaoingia katika mkutano huo wa uchaguzi kwa lengo la kupiga kura.

Tedy alisema kuwa mkutano huo wa uchaguzi mkuu utatanguliwa na agenda ya kupitisha katiba mpya ya ZFA ambayo imefanyiwa marekebisho katika vipengele mbalimbali.

"Hivi sasa tunaendelea na mchakato wa kupitisha katiba za vyama vya mikoa ili kupata wajumbe ambao moja kwa moja wataingia katika mkutano mkuu na pia ZFA itatangaza kamati ya uchaguzi wa chama chake," alisema Tedy.

Aliitaja mikoa mitatu ambayo katiba zao zimeshapitishwa kuwa ni pamoja na Kusini Pemba, Kaskazini Pemba na Mjini Magharibi kwa upande wa Unguja.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 26 | 20 | 4 | 2 | 43 | 17 | 64 |
| 2.AZAM | 26 | 15 | 8 | 3 | 36 | 17 | 53 |
| 3.SIMBA | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.KINONDONI MC | 28 | 9 | 14 | 5 | 31 | 18 | 41 |
| 5.LIPULI | 29 | 9 | 11 | 9 | 24 | 26 | 38 |
| 6.JKT TANZANIA | 29 | 8 | 12 | 9 | 17 | 18 | 36 |
| 7.ALLIANCE | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 8.MBAO | 28 | 9 | 9 | 10 | 19 | 26 | 36 |
| 9.MTIBWA SUGAR | 26 | 10 | 5 | 11 | 26 | 21 | 35 |
| 10.MBEYA CITY | 27 | 9 | 7 | 11 | 27 | 29 | 34 |
| 11.COASTAL UNION | 28 | 7 | 13 | 8 | 26 | 30 | 34 |
| 12.RUVU SHOOTING | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 13.KAGERA SUGAR | 27 | 7 | 12 | 8 | 21 | 25 | 33 |
| 14.MWADUI | 29 | 9 | 6 | 14 | 31 | 36 | 33 |
| 15.STAND UTD | 29 | 9 | 6 | 14 | 27 | 37 | 33 |
| 16.NDANDA | 27 | 8 | 9 | 10 | 17 | 27 | 33 |
| 17.TZ PRISONS | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18.SINGIDA UTD | 27 | 8 | 8 | 11 | 20 | 26 | 32 |
| 19.BIASHARA UTD | 27 | 5 | 9 | 13 | 18 | 29 | 24 |
| 20.AFRICAN LYON | 29 | 4 | 10 | 15 | 18 | 36 | 22 |

Michezo
Ijumaa Machi 8, 2019
Nipashe



## United kumtangaza Solskjaer mapema

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Manchester United, Romelu Lukaku (katikati), akijaribu kumtoka beki wa PSG, Thiago Silva (kushoto) na kufanikiwa kumfunga kipa wa timu hiyo, Gianluigi Buffon, katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. United ilishinda mabao 3-1 na kusonga mbele katika michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# ZAHERA: YANGA HATUTAYUMBA

● ● ● Kocha huyo afurahia kurejea nyota wake kikosini ambao...

**Na Faustine Feliciane**

NYOTA wanne wa Yanga waliokuwa majeruhi wamepona na wako tayari kurejea kuongeza nguvu katika kikosi cha kwanza cha kocha Mwinyi Zahera ambaye amesema kuwa hii itawaongezea kasi kwenye mbio zao za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA ambayo wametinga hatua ya robo fainali.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa wanajiwinda kuwavaa KMC katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Wachezaji waliorejea katika kikosi cha kwanza ni pamoja na Andrew Vincent 'Dante' na Thaban Kamusoko ambao hawakuonekana katika mechi iliyopita dhidi ya Alliance FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba na vinara hao kupata ushindi wa bao 1-0.

Zahera aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake sasa kiko kamili na hali hiyo inamweka katika nafasi nzuri kuelekea mchezo huo dhidi ya KMC yenye wachezaji mchanganyiko.

**"Wachezaji wote wanafanya mazoezi kwa pamoja, mchezo uliopita tuliwakosa Dante na Kamusoko ambao wote walikuwa majeruhi lakini sasa wamerudi na wanaweza kucheza mchezo ujao," alisema Zahera.**

Aliongeza kuwa anafurahishwa na ushindani uliopo katika mazoezi ya timu hiyo yanayofanyika kwenye Uwanja wa Chuo cha Polisi Kurasini jijini na hii inaonyesha kwamba kila mchezaji yuko tayari kupambana.

"Ukiangalia tupo kwenye hali nzuri, ushindi wa ugenini dhidi ya Alliance ulikuwa muhimu sana kwetu kuelekea katika mchezo wa Jumapili, tunataka kuendeleza kasi yetu ya ushindi," alisema Zahera.

Kocha huyo Mkongomani alisema kuwa hatua ambayo ligi hiyo imefikia ni ngumu na hakuna timu yoyote ambayo wataibeza kutokana na kila upande unahitaji kutimiza malengo yake kuelekea hatua ya lala salama.

Yanga yenye pointi 64 iko kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na Azam FC ambao wana pointi 53 wakati mabingwa watetezi, Simba wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 51, lakini wamecheza michezo sita pungufu dhidi ya Yanga na Azam.

Wakati huo huo, Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea leo kwa African Lyon kuivaa Tanzania Prisons na saa 1:00 usiku Azam FC watakaikaribisha JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi jijini.

## Simba kuwavaa Waalgeria tofauti

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA imebakia siku moja ili kufahamu nafasi ya wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Simba kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, amesema kuwa wamejipanga kuikabili JS Saoura kwa mbinu mbalimbali.

JS Saoura itawakaribisha Simba katika mechi ya Kundi D itakayochezwa kuanzia saa 4:00 usiku mjini Alexandria, wakati mchezo mwingine wa kundi hilo utaanza saa 1:00 kati ya AS Vita wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo watakapowavaa Al Ahly kutoka Misri.

Rweyemamu aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wote wako salama na hali ya hewa iliyoko Alexandria wameshaizoea kutokana na kufika katika mji huo kwa mara kadhaa.

Meneja huyo alisema kuwa wanatarajia kucheza tofauti na walivyocheza Dar es Salaam kutokana na kukosekana kwa baadhi ya nyota walioanza akiwamo mshambuliaji, Emmanuel Okwi na beki, Juuko Murshid.

"Mchezo huu ni wa pili, wachezaji wengi wanajuana, sisi tutakuwa na mabadiliko na wao tumeona wanamabadiliko katika mechi zao zilizopita, si kikosi kile kile tulichokifunga, ila tumejipanga na tunaamini tutapata kile tulichokifata," alisema meneja huyo.

HALI YA HEWA

Inaelezwa kuwa mchana hali ya hewa ya mchana ni ya joto kama ilivyo Dar es Salaam na jioni ndio huwa na baridi kali.

"Hakuna baridi kabisa muda wa mchana, ila usiku ndio kuna baridi, ila hali iko shwari," Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Mkuu wa msafara, Ahmed Mgoyi, aliliambia Nipashe kwa kifupi jana.

Baada ya mechi ya kesho, Simba itarejea jijini kuwasubiri AS Vita katika mchezo wa mwisho wa hatua hiyo ya makundi utakaochezwa Machi 16 kwenye Uwanja wa Taifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >